

**PM aipa neno KKKT ukamilishaji chuo SEKOMU**

UKURASA 2




**Yupi baba mzazi wa Diamond?**

UKURASA 20

**MAISHA**
Nipashe Baba, Mama na Mwana *Jumapili*



Ni mtoto wako lakini unazijua tabia zake?



MAISHA NI NYUMBA
Fondoo jinsi ya kupamba nyumba mitindo maarufu



HARUSI



SHINGO YA TWIGA
Maziwa mtindi, limao inatosha kuitengeneza

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Januari 17, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0580463
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mmiliki kampuni mikopo umiza aingia matatani



• **Adaiwa** kushikilia kadi 400 za benki... *Endelea Uk.2*




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikata utepe kuzindua kalenda ya Amani Milele, baada ya kufungua kongamano la pili la amani, jijini Zanzibar jana. Anayemsaidia ni Mwakilishi wa waandishi waliopata elimu ya amani, Abubakar Harith na (kushoto) ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Sheria, Katiba, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## Viongozi vikosi KMKM, Zimamoto, JKU wasimamishwa kazi

UKURASA 3

## Moto ulivyoteketeza hoteli 2 za kitalii Z'bar

UKURASA 2



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

MICHEZO SIMBA, YANGA ZASUBIRI MUDA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# PM aipa neno KKKT ukamilishaji chuo SEKOMU

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameutaka uongozi mpya wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Mashariki inayomiliki chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa (SEKOMU), ukamilishe mahitaji ambayo yataiwezesha Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), kukiruhusu chuo hicho kuendelea na udahili.

Alitoa kauli hiyo jana wakati alipokutana Askofu Mteule wa Dayosisi hiyo Mchungaji Dk. Msafiri Mbilu pamoja na viongozi wengine wapya waliochaguliwa. Kikao hicho kilifanyika katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Mlimwa.

Waziri Mkuu alisema hayo baada ya Askofu Dk. Mbilu kuiomba serikali iusaidie uongozi wa Dayosisi hiyo kukiwezesha chuo hicho kufunguliwa na kuruhusiwa kufanya udahili. Mwaka 2018 TCU ilikisitishia chuo hicho kufanya masomo na udahili wa wanafunzi katika ngazi zote baada ya kukosa vigezo.

"Kamilisheni mahitaji yatakayokifanya chuo chenu kiweze kuendelea kufanya udahili. Taarifa niliyonayo ni kwamba TCU walishakuja kukutana nanyi na kufanya ukaguzi, walitoa mahitaji kadhaa ambayo mnapaswa kuyakamilisha na nimesikia mmeridhia na kazi hiyo inaendelea."

Mbali na agizo hilo, pia Waziri Mkuu aliwashukuru viongozi wa dini nchini kutokana na mchango mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa taifa. "Viongozi wa dini ni watu muhimu sana, nchi imetulia na ina amani, hivyo kuwa kimbilio kwa waliokosa amani makwao."

Awali, Askofu Dk. Mbilu alimweleza Waziri Mkuu kwamba Chuo Kikuu cha SEKOMU kimezuiliwa kufanya udahili kutokana na changamoto mbalimbali za kimfumo wa ndani ya Dayosisi na ndani ya chuo ikiwa ni pamoja na kuwa na viongozi wa kukaimu kwa muda mrefu jambo ambalo kwa sasa tayari limeshapatiwa ufumbuzi.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni madeni makubwa yakiwamo ya mishahara ya watumishi, ambayo tayari uongozi umeshaanza kulipa malimbikizo hayo na wameweka mipango ya kumaliza kulipa madeni hayo. Pia, kiongozi huyo alisema chuo kimeshapata walimu wa kutosha chuo kitakapofunguliwa.

Askofu Dk. Mbilu alisema kabla ya kufungiwa Chuo Kikuu cha SEKOMU kilikuwa kinatoa elimu katika nyanja mbalimbali ikiwamo elimu maalumu ya kuwahudumia watu wenye ulemavu katika ngazi ya shahada na shahada ya uzamili, na kutoa wataalamu wengi.

# Mmiliki wa kampuni matatani tuhuma kushikilia kadi 400 za benki za watumishi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Dodoma inamtafuta mmiliki wa kampuni ya ukopeshaji fedha ya mjini Kondoa, Abubakary Kinyuma, baada ya kubainika kushikilia kadi za benki zaidi ya 400 za watumishi mbalimbali, wakiwamo wanaokaribia kustaafu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari Jijini hapa, Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, Sosthenes Kibwengo, alisema Taasisi hiyo pia inaichunguza kampuni ya mmiliki huyo, 'Geneva Credit Shop' baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi 30, wanaodaiwa kupatiwa mikopo umiza na kampuni hiyo.

"Uchunguzi wetu wa awali umeonyesha kwamba pamoja na kampuni hiyo kufanya biashara kwa zaidi ya miaka 25, lakini ilisajiliwa rasmi Oktoba 2016 na hivyo haikuwa inalipa kodi, tumebaini kwamba wengi wakopeshwaji ni watumishi wanaokaribia kustaafu na wamekuwa wakilipishwa riba kubwa kinyume na taratibu za nchi," alisema Kibwengo.

Alisema Kamati ya Usalama wa Wilaya ya Kondoa, ilifuatilia suala hilo na kufanikiwa kukamata kadi hizo zaidi ya 400 zikiwa zimeshikiliwa na mmiliki huyo ambaye wanamtafuta.

"Mfano mmoja wa walioilalamika kwetu alikopeshwa Sh. 350,000, lakini pamoja na kurejesha Sh. milioni 4.6 alipostaafu mwaka 2018, alikamatwa na mmiliki huyo na kutakiwa kurejesha zaidi ya Sh. milioni 35," alisema Kibwengo.

Alisema imebainika mmiliki huyo amekuwa na tabia ya kuwaandikisha wadeni wake mikataba kwa nguvu na baadaye kuipeleka mahakamani ili kuhalalisha madai yake.

Wakati huo huo, Taasisi hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, inatarajia kumfikisha mahakamani, Mhasibu Msaidizi wa Mapato wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Severo Mutegeki (42), kwa tuhuma za kuisababishia mamlaka hiyo hasara ya Sh. milioni 428.

Alisema mtuhumiwa huyo atafunguliwa shauri la uhujumu uchumi, atashtakiwa kwa makosa matatu ya matumizi mabaya ya mamlaka.

"Uchunguzi wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, umeonyesha kwamba kati ya Julai na Novemba 2015, mtuhumiwa alishindwa kuzingatia kanuni za fedha za DUWASA na kufuja sehemu ya maduhuli yaliyokusanywa badala ya kuyawasilisha benki," alisema.



Sehemu ya mabaki ya majengo ya hoteli ya Ocean Paradise, baada ya kuteketea kwa moto huko Zanzibar jana alfajiri.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Moto ulivyoteketeza hoteli 2 za kitalii

**Na Waandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WATALII 129 wamenusurika kifo eneo la Pwani Mchangani, Mkoa wa Kaskazini Unguja visiwani Zanzibar, baada ya hoteli mbili kuteketea moto jana.

Akizungumza na Nipashe, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Leila Mohamed Mussa, alisema moto huo ulianza kuwaka katika chumba cha ufundi katika hoteli ya Ocean Paradise, kisha kusambaa katika vyumba vya kulala wageni katika hoteli ya jirani ya Tui Blue.

Alisema moto huo ulianza majira ya saa nane usiku katika hoteli ya Ocean Paradise, kisha kusambaa na kusababisha hoteli nyingine ya Tui Blue nayo kuungua.

Waziri huyo alisema, moto huo umeteketeza mgahawa wa hoteli hiyo, ofisi za utawala, majengo 13 ya hoteli ambayo ndani yake kuna vyumba vinane vilivyokuwa na wageni wamelala.

Alisema upepo mkali katika eneo la tukio ulisambaa katika hoteli ya Tui Blue na kusababisha hasara kubwa ya kuungua vyumba vya hoteli hiyo.

"Moto ulikuwa mkubwa na hii ilitokana na upepo mkali ulokuwapo hususani na kule ni maeneo ya pwani na kama unavyojua maeneo ya bahari ikifika majira ya usiku upepo unakuwa mkubwa, hoteli nyingi za kitalii zinaezekwa kwa makuti, hivyo inakuwa rahisi moto kusambaa kwa haraka," alisema Leila.

Alisema watalii wote ambao walikuwa katika hoteli hizo walifanikiwa kutoka salama kwa kukimbilia katika eneo la fukwe ya bahari pamoja na mali zao.

"Wageni wa hoteli waliondolewa na kupelekwa katika eneo la fukwe wakiwa salama, hoteli ya Tui blue ilikuwa na wageni 209 wote na mali zao wapo salama na tayari wameshapelekwa katika hoteli zingine," alisema Leila.

Alilishukuru Jeshi la Zimamoto Zanzibar kwa jitihada za kuzima moto huo, ili kuepuka athari zaidi kwa maeneo mengine, licha ya kuwapo kwa upepo mkali.

Kamanda wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Haji Mohammed, alisema chanzo cha ajali hiyo bado hakijajulikana, lakini uchunguzi wa awali unasadikiwa kuwa ni hitilafu ya umeme.

Kuhusu hasara iliyopatikana, Kamanda Mohammed alisema bado haijafahamika.

**•Imeandaliwa na Rahma Suleiman na Hawa Andallah**

HABARI KITAIFA

# Dereva taxi afariki kwa kusombwa maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

DEREVA taxi katika Jiji la Dodoma, Maxmilian Richard, amefariki dunia akiwa ndani ya gari lake, baada ya kusombwa na maji wakati akivuka korongo.

Dereva huyo aliyekuwa mkazi wa eneo la Nzuguni alisombwa na maji yaliyotokana na mvua inayoendelea kunyesha alipokuwa akivuka korongo linalounganisha eneo la Nzuguni A na B, jijini hapa.

Akizungumza na Nipashe, Diwani wa Kata ya Nzuguni, Aloyce Luhega, alisema alipigiwa simu majira ya saa 9:30 usiku na mmoja wa wananchi iliyoeleza kwamba kuna gari limesombwa na maji likiwa na mtu ndani.

Diwani Luhega alisema baada ya kupokea taarifa hiyo alipiga simu polisi na Mkuu wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Dodoma alituma askari na kukaa eneo la tukio kwa takribani saa sita wakisubiri maji kupungua.

Alisema baada ya maji kupungua tairi za gari zilianza kuonekana ndipo wananchi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walifanikiwa kuutoa mwili wa marehemu pamoja na gari.

Luhenga aliitoa wito kwa wakazi wa eneo hilo hasa kipindi hiki cha mvua kuwa makini pale wanapoona maji yamejaa kutojaribu kuvuka bila kuchukua tahadhari. "Naomba wananchi wachukue tahadhari katika kipindi hiki cha mvua, kwa sababu hakuna anayejua kina cha maji, hivyo ni vyema kusubiri mvua ikatike ndipo uendelee na safari," alisema Luhega.

Kadhalika, aliiomba serikali kuendelea kurekebisha miundombinu katika maeneo hayo, ili kuchepusha mikusanyiko ya maji hususani kipindi cha mvua.

Hivi karibuni, Nipashe ilichapisha habari kuhusu wakazi wa Nzuguni kuiomba serikali kuwajengea daraja linalounganisha mitaa ya Nzuguni A na B kwenye korongo hilo, kutokana na kuhatarisha maisha yao wakati wa mvua.



Wananchi wakiangalia gari dogo aina ya taxi, lililosombwa na maji wakati dereva wake akivuka korongo linalounganisha eneo la Nzuguni A na B, jijini Dodoma juzi. Dereva wa gari hilo, Maxmilian Richard, alifariki Dunia katika tukio hilo. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# 'Msikurupuke kununua ardhi Dodoma mtanunua makaburi'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, amewatahadharisha wananchi kutoka mikoa mbalimbali wanaokimbilia kununua ardhi isiyopimwa katika Jiji hilo, kuwa makini kuuziwa maeneo ya makaburi.

Alitoa tahadhari hiyo wakati wa kikao kilichowakutanisha wakuu wa taasisi za kiserikali za jiji hilo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alikuwa akipokea taarifa ya mipango ya upelekaji huduma kwenye maeneo ya uwekezaji na yanayojengwa kwa kasi jijini humo.

Alisema hivi sasa kuna wimbi la watu kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, wanakimbizana maporini kununua ardhi ambayo haijapimwa.

Mafuru aliwataka watambue kuwa Jiji la Dodoma lina ramani yake ya mipango miji ya miaka 20 na hakuna ardhi ambayo haina matumizi.

"Msikurupuke kununua mtanunua makaburi, msikurupuke mkanunua mtanunua msitu, bahati mbaya sana kuna wataalamu juzi walikuwa wanazungumza wakadhani siwasikii wamesha-nunua chanzo cha maji Makutupora hiyo imekula kwao," alisema Mafuru na kuongeza:

"Waje waulize kabla ya kufanya maamuzi yoyote ya ardhi, waje tuangalie, ununuaji wa holela wa Jiji la Dar es Salaam au Mwanza kwa Dodoma ni ngumu, master plan (mpango mji) tuliyonayo ni ya miaka 20 na ndiyo kwanza tupo mwaka wa kwanza," alisema Mafuru.

Alisema kwa sasa kuna upimaji unaendelea kwenye maeneo mbalimbali na ifikapo Juni, mwaka huu Jiji la Dodoma litakuwa limezifikia kata zote 41 katika upimaji wa maeneo, ili wananchi wajenge kwenye viwanja vilivyopimwa.

Kadhalika, alisema madalali wa ardhi waliopo Jiji la Dodoma wengi wao ni wataalamu wa ardhi wastaafu waliokuwa kwenye Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA), wana taarifa lakini ambazo siyo za kweli.

"Kabla hujanunua kiwanja chochote uje kuangalia kwenye mfumo inamsoma nani, ili tukujibu endelea, lakini tatizo lipo wateja wetu wengi wanakuja kuangalia wakati walishalipa inakuwa kesi."

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk.Binilith Mahenge, aliwataka wananchi kuzingatia maelekezo ya Mkurugenzi huyo, kujiridhisha kuhusu uhalali wa eneo husika.

Dk. Mahenge alisema: "Kwenye ujenzi holela msiweke alama ya 'X' bomoeni kabisa maana mnapoweka alama ya 'X' wao wanaendelea na mwisho wa siku nyumba inasimama mnapelekana mahakamani, kama amekosea ondoa mara moja."

Akisoma maazimio ya kikao hicho, Katibu Tawala Msaidizi anayesimamia miundombinu Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Happiness Mgalula, alisema Jiji linatakiwa kuainisha maeneo matatu ya kipaumbele katika uwekezaji, ili taasisi nyingine zijipange kupeleka huduma na kuwafanya wawekezaji kuwekeza.

## Viongozi vikosi vya ulinzi wasimamishwa kazi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADHI ya viongozi wa vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wamesimamishwa kazi kutokana na uchunguzi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) kuhusu ubadhirifu wa fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Miongoni mwa waliosimamishwa kazi kwa tuhuma mbalimbali za ubadhirifu wa mali za umma ni Naibu Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, Haji Gora Haji.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu kusimamishwa kazi kwa watumishi hao, Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masod Ali Mohammed, ofisini kwake Vuga, alisema watumishi hao amewasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi wa kadhia hizo.

Alisema taarifa za awali za uchunguzi wa ZAECA zimeleza, Naibu Kamishna huyo anakabiliwa na tuhuma za upotevu wa fedha za umma zilizohusisha mradi wa ujenzi wa jengo la Kituo cha Zimamoto na Uokozi huko Kijichame, Kisiwani Pemba.

Alisema kadhia zingine ni usimamizi usioridhisha wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na kikosi hicho na kadhia ya zoezi lenye ukakasi la upigaji wa picha kwa askari wa watumishi katika kikosi hicho.

Aidha, alisema wengine aliowasimamisha kazi katika kikosi hicho ni Mhasibu Mkuu wa kikosi hicho, Mgeni Rajab Miraji na Mkuu wa Utumishi wa kikosi hicho, Sihami Juma Kombo, kutokana na kadhia mbalimbali zinazowakabili ikiwamo tuhuma za makato ya fedha za askari kwa sababu zisizo na msingi. Pia, amewasimamisha kazi Mkuu wa Utawala wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Mussa Mohamed Shaame, ili kupisha uchunguzi kuhusu zoezi lenye ukakasi la upigaji wa picha kwa askari na watumishi katika jeshi hilo.

Waziri huyo pia alimsimamisha kazi Mhasibu Mkuu wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar, Haji Maulid, kwa tuhuma za ubadhirifu zilizowasilishwa na ZAECA na pia amemsimamisha kazi Mkuu wa Bohari Kuu wa Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM), pamoja na msaidizi wake.

Alisema ni bora kuwa na watendaji wachache wanaowajibika kuliko kuwa na kundi kubwa la watendaji wasiowajibika na kutumia vibaya mali za umma.

"Ni vyema fedha za serikali kuziogopa kama sumu na kila mmoja awajibike kwa vitendo ili nchi ipate maendeleo na kukemea vitendo vya rushwa na ufisadi," alisema.

HABARI KITAIFA

# Mmiliki afunguka bucha nyamapori kufungwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUCHA ya nyamapori iliyozinduliwa mwishoni mwa mwaka jana jijini hapa, limeshindwa kutoa huduma iliyotarajiwa, huku mmiliki wa bucha hiyo akifunguka kilichomkwamisha.

Nipashe ilitembelea bucha hiyo jana iliyopo katika mtaa wa Chang'ombe na kukuta likiwa limefungwa huku wananchi wanaoishi jirani wakieleza kuwa tangu ilipozinduliwa mwaka jana, hakuna kitoweo kilichopelekwa kwa ajili ya kuuzwa.

Mmoja wa wananchi hao, Omari Bakari, alisema siku ya kwanza ambayo ndiyo ulikuwa uzinduzi wa bucha hiyo, nyama ya swala iliuzwa kwa wingi, wananchi kutangaziwa kuwa kesho yake nyama ya wanyama pori wengine itakuwapo.

"Sasa tangu siku hiyo imekuwa ni kero kwetu wanakuja watu kila siku kuuliza, yani tumechoka hata kuwajibu wateja wanaokuja, naona hii biashara walikuwa hawajajipanga kuifanya," alisema Bakari.

Alisema kumekuwapo na mwitikio mkubwa wananchi kuhitaji nyamapori, lakini kila wakifika katika bucha hiyo wanakuta limefungwa na hakuna mtu wa kueleza sababu.

Salum Makinga, alisema kuna mwitikio mkubwa wa wateja wanaohitaji nyamapori na kwa siku wanafika watu zaidi ya 100 kutoka mikoa mbalimbali wakiwa na magari wakiulizia nyama hiyo.

Aliomba kutolewa kwa matangazo ya kutokuwapo kwa huduma hiyo hadi watakapo jipanga.

"Siku ya uzinduzi watu walikuwa wengi na iliuzwa kilo kwa Sh. 5,000 na tukaambiwa mzigo ukija tena kilo itakuwa Sh. 8,000 kwa minofu tupu ni Sh. 10,000, sasa hivi tunawajibu watu wachukue namba yao hapo juu kwenye bango waulize maana imekuwa wakijibu wanaleta na hawaleti," alisema Makinga.

Nipashe ilimtafuta mmiliki wa bucha hiyo, Samson Kitangengi na kueleza tatizo lililosababisha kushindwa kutoa huduma kuwa ni kupewa kibali cha uwindaji eneo ambalo halina wanyama.

Alisema amepangiwa kuwinda kwenye kitalu Simbangulu, na Sikonge mkoani Tabora ambavyo vimeingiliwa na shughuli za binadamu.

"Hata siku tuliyozindua bucha, mimi nilizunguka kwenye maeneo ambayo nimeruhusiwa nikakosa, ndipo Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), wakaja na nyama hizo wenyewe, maana kila eneo nililopangiwa nikifika sipati wanyama kutokana na kuvamiwa na shughuli za kibinadamu," alisema Kitangengi.

Alisema ameandika barua kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia TAWA, amejibiwa kwamba Januari 19, mwaka huu ahudhurire kikao jijini Arusha ambacho kitawajumuisha wauza wengine.

"Juzi nilienda Tabora mvua zimenyesha unaingia porini unakwama na wanyama hawaonekani, baada ya kutoa malalamiko ndiyo tukaitwa, hivyo nina imani mwishoni mwa wiki majibu yatajulikana kuhusu hatima ya bucha hilo," alisema.

Aliwaomba wateja kuwa wavumilivu wakati akisubiri majibu ya serikali iwapo watabadilishiwa vitalu. Desemba 20, mwaka jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TAWA, Meja Jenerali mstaafu, Hamis Semfuko alizindua bucha ya kwanza ya nyamapori nchini, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli alilolitoa mwaka jana la kuanzisha bucha za kuuza nyama hiyo.

Bucha hiyo inamilikiwa na Kampuni ya Kitangengi Enterpress mtaa wa Chang'ombe, jijini Dodoma na ni ya kwanza kati ya 46 zilizopata usajili baada ya kamati ya kumshauri Kamishna kuhusu kuuza nyamapori kuridhia.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (katikati) akiongoza dua ya kumwombea Rais John Magufuli afya njema, amani ya nchi na marehemu katika familia yake waliofariki miaka mitano iliyopita, iliyofanyika katika kijiji cha Mwera, wilayani Pangani, mkoani Tanga jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Taasisi vinara wa rushwa hadharani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani Dodoma imezitaja sekta sita vinara wa rushwa mkoani humo, huku eneo la serikali za mitaa likiongoza likifuatiwa na mikopo umiza.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu taarifa ya utendaji wa taasisi hiyo kwa robo ya Oktoba hadi Desemba, mwaka jana, alizitaka sekta hizo kuwa ni pamoja na Serikali za Mitaa ambayo imelalamikiwa kwa asilimia 23, ya pili ni mikopo umiza asilimia 20, ya tatu ni sekta ya ardhi asilimia 14, huku vyama vya siasa au uchaguzi, polisi, afya zikilalamikiwa zote kila mmoja kwa asilimia sita.

Taasisi hiyo pia imebaini baadhi ya kampuni za ujenzi wa miundombinu ya barabara na maji mkoani humo kukwepa kodi ya ushuru wa huduma, hali inayozikosesha halmashauri mapato stahiki.

"Kwa mfano tumebaini kwamba Sh.milioni 500 hazikulipwa na kampuni hizo kati ya mwaka 2017 hadi 2020, TAKUKURU kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) imeanza kufuatilia ili fedha hizo zilipwe," alisema Kibwengo.

Kwa kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu, alisema TAKUKURU imeweka mkazo kuchunguza ubadhirifu wa fedha za umma, hususani zinazotolewa kama mikopo ya taasisi, vyama vya ushirika na watu binafsi.

Pia, wataanza kufuatilia fedha za kodi ya ushuru wa huduma ambazo zilipaswa kulipwa na kampuni, lakini hazikufanya hivyo.

# Mbaroni madai kumhonga Mganga Mkuu Serikali kupata cheti cha corona

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imemkamata raia wa Kenya, Alexander Mwikali (42), kwa tuhuma ya kutoa rushwa ya Sh. 200,000 kwa Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, ili ampatie cheti cha uthibitisho wa kutokuwa na ugonjwa wa corona.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, raia huyo anayeishi Nkuhungu, jijini hapa, anafanya kazi kama mtaalam wa nyama Kampuni ya Alkafil.

Kibwengo alisema raia huyo alinaswa baada ya kuandaliwa mtego ofisini kwa Mganga Mkuu.

"Mwikali alikuwa akitoa rushwa ya Sh. 200,000 kinyume na kifungu namba 15(1) (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na rushwa namna 11 ya mwaka 2007, kwa kumshawishi ili apate cheti hicho," alisema Kibwengo. Alisema mtuhumiwa huyo alifikishwa Mahakama ya Mkoa wa Dodoma na kufunguliwa shtaka husika ambalo alikiri na kutozwa faini ya Sh. 500,000, huku fedha aliyotoa kama hongo ikitaifishwa.

Katika hatua nyingine, Kibwengo alisema TAKUKURU inawashikilia wanafunzi 13 wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) Dodoma kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya rushwa na udanganyifu, wakati wa kufanya mtihani wa marudio wa somo la Applied Statistics II, kwa mwaka wa tatu uliofanyika Novemba, mwaka jana.

Kibwengo alisema: "Uchunguzi wa awali umeonyesha kuwa wanafunzi hao, kwa kutumia rushwa walirudia kufanya mtihani huo nje ya chumba cha mtihani na baadaye wakajaribu kuingiza karatasi za kujibia mtihani kwenye mfumo rasmi, lakini chuo kikawabaini na kutoa taarifa kwetu".

Aliwataka waliokuwa wanafunzi wa chuo hicho, Evarist Nyaki na Lameck Kawinga, kuripoti katika ofisi za TAKUKURU ili kusaidia uchunguzi wa tukio hilo.

Kadhalika, Kibwengo alisema TAKUKURU imeokoa Sh. milioni 283.9, viwanja 14 na shamba moja la ekari tano.

Alisema fedha hizo zimetokana na mikopo umiza iliyorejeshwa kwa wananchi wanyonge zilizolipwa kinyume na utaratibu, madeni ya vyama vya akiba na mikopo na mishahara hewa.

HABARI KITAIFA



Wakazi wa Magole, Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam, wakipita katika daraja lililoharibika kwa muda mrefu sasa bila kufanyiwa ukarabati, kitendo kinachowasababishia usumbufu hasa nyakati za mvua. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DC Joketi aagiza watendaji TANESCO kuswekwa ndani

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, Jokate Mwegelo, ameagiza kuswekwa mahabusu baadhi ya watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wilayani humo, baada ya kukithiri kwa malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu utolewaji wa huduma duni.

Alitoa agizo hilo baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika ofisi za TANESCO Wilaya ya Kisarawe na kukuta idadi kubwa ya wananchi waliofika kutoa malalamiko kutokana na kukosa huduma ya nishati ya umeme kwa wakati.

Akizungumza katika ofisi hizo, Jokate alisema hawezi kukubali kuona wananchi wakiendelea kulalamika kuhusu kukosa huduma ya umeme, huku baadhi ya watendaji wakipuuza na kuwadharau wananchi.

Alisema sababu kubwa ya kuwapo kwa malalamiko mengi ya wananchi inatokana na kukithiri kwa vitendo vya rushwa kwa baadhi ya watendaji na watumishi wa TANESCO.

"Kuna watendaji wanapenda rushwa na matokeo yake wanakwamisha huduma kupatikana kwa wakati unaotakiwa," alisema Joketi huku akitoa amri kwa polisi kuwakamata baadhi ya watendaji na watumishi wa Shirika hilo na kuwaweka rumande wajitafakari wakiwa huko.

"Wanaohusika wote na kutoa huduma kwa wateja wapelekwe kituo cha polisi watafakari utendaji wao wa kazi na maisha yao."

"Haiwezekani wananchi wawe wanalalamika kila siku kuhusu huduma za TANESCO hapa Kisarawe, tumekuwa tukizungumza mara nyingi kwenye vikao vyetu, lakini wenzetu hamtaki kusikia wala hamfanyii kazi malalamiko ya wananchi," alisema Joketi na kuongeza:

"Sasa niwaambie mimi niko na wananchi, malalamiko ni mengi, tunakubaliana na humfanyi kazi, nachukua haya malalamiko na kuyafikisha kwa Mtendaji Mkuu wa TANESCO maana ninyi hapa mmeshindwa kuyafanyia kazi, huduma kwa wateja mbovu," alisema Joketi.

Akitoa mfano, Joketi alisema kuna mmoja wa mwananchi ambaye anaishi karibu na ofisi za TANESCO na alipopata tatizo la hitilafu ya umeme kwenye nyumba yake ilichukua zaidi ya mwezi mmoja pasipo kupata msaada wowote.

"Shida ya hapa ni nini? Wananchi wako wengi na wote wanalalamikia TANESCO, Meneja kaa na timu yako muondoe kero za wananchi, nataka nipate taarifa jinsi ambavyo mmeshughulikia hizi kero zote na wote walioko hapa nataka wapate huduma leo leo, mtafanyaje mtajua wenyewe," alisema Joketi.

Alisema kuna haja ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi katika ofisi za TANESCO Wilaya ya Kisarawe ili kukomesha rushwa alizodai zinatolewa kwa baadhi ya watumishi wa shirika hilo.

# Mzee wa Upako ammwagia sifa Dk. Mwinyi

**Na Thobias Mwanakatwe**

MCHUNGAJI wa Kanisa la Maombezi (GRC) la jijini Dar es Salaam, Anthony Lusekelo, maarufu Mzee wa Upako amemmwagia sifa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi kwa jitihada za kuwaunganisha Wazanzibari.

Alitoa pongezi hizo juzi mkoani Mbeya wakati akihojiwa na moja ya kituo cha habari, akiwa katika msiba wa mjomba wake, Mchungaji Mbokigwe Mwalwajo.

Akizungumza na kituo hicho, Mchungaji Lusekelo alimpongeza Dk. Mwinyi kwa jitihada hizo, akishauri jitihada hizo zifanyike pia Tanzania Bara.

"Tulikuwa katika uchaguzi, umetugawa kidini, kikabila na kikanda, huku Tanzania Bara tuendelee kuwaunganisha Watanzania kama inavyofanyika Zanzibar, tuponye majeraha ya uchaguzi ili tuwe wamoja," alisema.

Kadhalika, Mchungaji Lusekelo alisema viongozi na wananchi hawana budi kumsaidia Rais John Magufuli, ili atekeleze ahadi ambazo aliwaahidi Watanzania wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu.

"Rais Magufuli alizungumza bungeni kwa mara ya kwanza wakati analizindua kwamba atawawezesha Watanzania kuwa mabilionea, Roma haikujengwa siku moja hiyo ndiyo azma ya Rais, kwa hiyo lazima tumwamini rais wetu," alisema Mchungaji Lusekelo.

Alisema miaka mitano ya uongozi wa Rais Magufuli Watanzania watarajie mambo mazuri ya maendeleo na uchumi kukua kwa kasi. Kuhusu viongozi wa dini kujiingiza katika siasa, Mchungaji Lusekelo alisema: "kimsingi huwezi kutenganisha siasa na dini sababu yote ni masuala ya kijamii."

"Kiongozi wa dini anatibu roho, siasa inatibu kimwili kama maji na umeme, kwa hiyo akiingia bungeni kule Mchungaji au Baba Askofu maana yake atawasaidia mara mbili wananchi kiroho na katika kuwaletea huduma za kijamii."

# Mbunge atoa msaada wa milioni 13/- kwa wanafunzi wenye ulemavu

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, amekabidhi vifaa vya shule vyenye thamani ya Sh. milioni 13 kwa wazazi na walezi wa wanafunzi 62 wenye ulemavu wa viungo.

Wanafunzi hao wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule za Manispaa ya Morogoro.

Miongoni mwa vifaa alivyokabidhi ni pamoja na madaftari, viatu, mabegi, sare za shule, kalamu na fedha. Akikabidhi msaada huo, Abood alisema: "Nimeamua tuanze na hawa wachache 62, lakini huu ni msaada ambao tumeutoa kwa wale wenye uhitaji mkubwa zaidi tumezingatia shida za hawa wananchi."

Mbunge huyo aliwaasa wazazi na walezi wa watoto hao kuwasimamia katika masomo, mwalimu awe mtu wa kati katika kufanikisha maendeleo ya watoto hao. "Nawaomba wazazi na walezi wasimamieni watoto wenu katika masomo, mwalimu awe mtu wa kati, fuatilieni taaluma za watoto wenu, mwalimu atamlea mtoto shuleni, lakini nyumbani mzazi una wajibu wa kutimiza majukumu yako" alisema Abood.

Alisema serikali inahitaji kuona kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule anapata fursa ya kusoma, ndiyo maana imeanzisha sera ya elimu bure kuanzia elimu ya msingi hadi sekondari. Baadhi ya wazazi na walezi ambao watoto wao wamenufaika na msaada huo kwa nyakati tofauti, walimshukuru mbunge huyo kwa kuonyesha moyo wa upendo na huruma ya kuwasaidia watu wanyonge na wenye vipato duni.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari ununuzi holela ardhi isiyopimwa ni muhimu

**KUMEKUWA** na tabia ya baadhi ya wananchi kila kunapotokea fursa kwenye mkoa fulani kukimbilia kwa lengo la kuwekeza ili baadaye wanufaike.

Toka serikali ihamishie makao makuu Dodoma na kuufanya mkoa huo kuwa jiji, kumekuwa na mwamko mkubwa wa wananchi kutafuta fursa za uwekezaji ikiwamo ardhi.

Baadhi ya wanaotafuta fursa hizo wameanza kudiriki kununua hata maeneo ambayo hayajapimwa bila kujua kufanya hivyo kutaleta athari kwa upande wao baadaye.

Katika kukomesha hilo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, amewatahadharisha wananchi kutoka mikoa mbalimbali wanaokimbilia kununua ardhi isiyopimwa katika jiji hilo kuwa makini na kwamba wanaweza kununua maeneo ya makaburi.

Wimbi la watu kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, ndio wanaoonekana kukimbizana maporini kununua ardhi ambayo haijapimwa.

Katika tahadhari hiyo Mkurugenzi amewataka kutambua kuwa Jiji la Dodoma lina ramani yake ya mipango miji ya miaka 20 na hakuna ardhi ambayo haina matumizi.

"Msikurupuke kununua mtanunua makaburi, msikurupuke mkanunua mtanunua msitu, bahati mbaya sana kuna wataalamu juzi walikuwa wanazungumza wakadhani siwasikii wameshanunua chanzo cha maji Makutupora hiyo imekula kwao."

Wamekumbushwa kuuliza kabla ya kufanya uamuzi wowote wa kununua ardhi kwa kutakiwa kwenda kuangalia kwa watu wa mipango miji.

Mikoa ambayo imeshamiri kwa ununuzi holela wa ardhi imetajwa kuwa ni Jiji la Dar es Salaam na Mwanza, hali inayofanya majiji hayo kutokuwa na mipango mizuri ya miundombinu.

Kwa upande wa Dodoma, tayari kuna mipango miji ya miaka 20 ijayo na ndiyo mwaka wa kwanza umeanza.

Pia, kuna upimaji unaendelea kwenye maeneo mbalimbali na imeelezwa kuwa Juni, mwaka huu Jiji la Dodoma litakuwa limezifikia kata zote 41 katika upimaji wa maeneo ili wananchi wajenge kwenye viwanja vilivyopimwa.

Wanaochangia ununuzi holela wa ardhi wametajwa kuwa ni wataalamu wa ardhi wastaafu waliokuwa kwenye Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA), ambao wana taarifa, lakini ambazo siyo sahihi.

Cha muhimu ni watu kuzingatia tahadhari iliyotolewa ya kutonunua kiwanja chochote bila kwenda kuangalia kwenye mfumo inamsoma nani.

Hata hivyo, imebainika kuwa wateja wengi wanakwenda kuangalia kwenye mfumo baada ya kuwa wameshalipia viwanja hivyo na kusababisha tatizo.


Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewataka wananchi kuzingatia maelekezo ya Mkurugenzi huyo, kujiridhisha kuhusu uhalali wa eneo husika.

"Kwenye ujenzi holela msiweke alama ya X, bomoeni kabisa maana mnapoweka alama ya X wao wanaendelea na mwisho wa siku nyumba inasimama mnapelekana mahakamani, kama amekosea ondoa mara moja."

Jiji la Dodoma linatakiwa kuainisha maeneo matatu ya kipaumbele katika uwekezaji kuwezesha taasisi nyingine zijipange kupeleka huduma na kuwavutia wawekezaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Mbegu hizi za mihogo zinaweza kumkomboa mkulima kiuchumi



Na Sabato Kasika

**TANZANIA** inatajwa kuwa miongoni mwa nchi zilizojaliwa kuwa rasilimali nyingi ambazo kama zikitumika inavyotakiwa, zinaweza kusaidia wananchi wake kuondokana na umaskini.

Moja ya baraka hizo ni kuwa na ardhi yenye rutuba, maji, mito na maziwa na Watanzania wakitumia rasilimali hizo kwa kuunganisha na nguvu kazi, uwezo na mitaji yao, wanaweza kupaisha uchumi wao na wa nchi kwa ujumla.

Ardhi hiyo inafaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali ikiwamo mihogo ambayo sasa inaelezwa kuwa ina soko kubwa nchini China, ambako kuna mahitaji makubwa ya zao hilo.

Hapa nchini, inaelezwa kuwa kuna zaidi ya aina 45 za mbegu za mihogo, lakini zaidi ya asilimia 80 ya mbegu hiyo ni ya asili, hali inayoonyesha kuwa wakulima wengi hawatumii mbegu bora za kisasa.

Mihogo ya asili inayotajwa na wataalam wa kilimo ni ile iliyolimwa miaka mingi iliyopita na kurithiwa vizazi hadi vizazi ikiwa na sifa mbalimbali kama kutoa mavuno madogo kwa hekta, huku mingi ikichukua muda mrefu kukomaa na inahifadhika shambani kwa muda mrefu bila kuoza.

Sifa nyingine ya mihogo hiyo ni kushambuliwa na magonjwa kama ugonjwa wa michirizi ya ki-kahawia, batobato na blaiti, na pia hushambuliwa na wadudu aina ya 'milibagi'.

Lakini wataalam wa kilimo wamekuja na mbegu mpya za zao hilo ambazo zinastawi katika kanda mbalimbali na kutoa mavuno mengi na kuwezesha wakulima kupata chakula cha kutosha na hata cha kuuza.

Baadhi ya mbegu hizo zilizoibuliwa na watafiti zinatajwa kuwa ni mkombozi, kyaka, meremeta, kiroba, nyakafulo, suma belinde, kasala, rangimbili, chereko, kizimbani na mumba.

Kituo cha Utafiti wa Mazao ya Kilimo cha Naliendele, Mtwara na vingine vya utafiti wa mazao ya kilimo, vilishafanya utafiti na kubaini mbegu hizo bora za mihogo zinazokomaa mapema.

Kwa mfano, katika Kanda ya Ziwa Victoria, inaelezwa kuwa mbegu ya mkombozi inastawi kwa wingi na ina uwezo wa kutoa mavuno mengi na pia kukinzana na ya magonjwa batobato na michirizi ya ki-kahawia.

Mbegu hiyo pia hukomaa kati ya miezi minane hadi 12, na kila hekari moja, mkulima anaweza kuvuna magunia ya mihogo kati ya 16 hadi 20 tofauti na mbegu za asili, ambazo hutoa magunia kati ya matano hadi sita kwa ekari.

Kutokana na hatua hiyo ya kuwapo kwa mbegu bora za mihogo ni la muhimu sasa wakulima wakapewa elimu zaidi ili waachane na ya zamani na kugeukia ya kisasa inayoweza kuwaongozea chakula na kuinua kipato chao.

Wataalam wa kilimo hawana budi kuwaelekeza wakulima aina bora za mbegu zenye ukinzani wa magonjwa na wadudu waharibifu, ili wazitambue na kuzichangamkia.

Hiyo ni fursa kwao, hasa kutokana na ukweli zinastahimili ukame, hivyo kwa kilimo cha hapa nchini cha kutegemea msimu wa mvua, bado watakuwa na uhakika wa kupata mavuno mengi.

Kila kanda ina mbegu zinazostawi kwa wingi, hivyo ili wakulima waweze kupata mavuno ya kutosha na hata kufanikiwa kupeleka mengine China, ni vyema kuelimishwa na kuachana na mbegu za zamani.

Kwa mfano, katika Kanda ya Ziwa, hasa Wilaya ya Musoma, wakazi wake wanajihusisha na kilimo hicho kwa ajili ya chakula na biashara, lakini kuanzia miaka ya 80 lilishambuliwa na ugonjwa uitwao 'milibagi'.

Tangu wakati huo, kilimo cha mihogo kimekuwa cha kusuasua, lakini tayari wakulima wamekuwa wakisambaziwa mbegu ya mkombozi, ili kuimarisha upya kilimo hicho.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Musoma, Godfrey Katima, anasema, mbegu za mkombozi ambazo husambazwa wilayani mwake, hasa Musoma Vijini, zimeonekana kustawi na kuleta matumaini kwa wakulima.

Anasema, wilaya hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali akiwamo Mbunge Prof. Sospeter Muhongo, wamekuwa wakisambaza mbegu hizo tangu mwaka 2016 ili kunufaisha wakulima.

Muungwana anaamini kwamba, kwa kuwa kilimo ni ajira na ni uchumi, wakulima hawana budi kuendelea kuelimishwa walime inavyotakiwa ili wapate mazao kwa ajili ya chakula na hata ya kuuza.

## FIKRA MBADALA



Nkwazi Mhango, Canada

# Siku Trump alipoivua nguo Marekani

**Baada ya shambulizi hili la aibu na hatari, maseneta na wabunge walirejea Capitol Hill na kumaliza kupitisha ushindi wa Biden. Walivamia wakiwa chini ya uenyekiti wa Makamu wa Rais Pence huku usalama wake, familia yake na wabunge ukiwa hatarini.**

ZIKIWA zimesalia wiki mbili kwa Rais wa Marekani, Donald Trump, anayemaliza muda wake, kuondoka Ikulu Jumba Jeupe (White House), hali ilichacha na kuchafuka kweli kweli. Mnamo Januari 6, 2021 ilikuwa "siku ya kiza" (rais mteule Joe Biden) na simanzi katika historia ya Marekani.

Kwani ni siku ambapo Rais wa Marekani alianzisha maasi dhidi ya taifa hili lenye kujivunia mizizi ya kidemokrasia huku likijiteua kuwa polisi wa demokrasia duniani.

Akiwa ameshindwa uchaguzi mkuu wa Novemba, 2020 na Biden, alikataa kumtambua, kumpongeza wala kukubali ushindi huu, Trump aliamua kufanya kile ambacho walatini huita sacriligo (sina tafsiri) au tuseme kilihataji kiasi fulani cha uchizi. Kutokana na hili, Wamarekani walitaka Trump aondolewe ofisini haraka ili Makamu wake wa Rais, Mike Pence amalizie ngwe yake.

Wengi wanajua namna Trump alivyohutubia mkutano wa hadhara muda mfupi kabla ya kuwahimiza wahuni na wabuguzi wa kimarekani kuvamia jengo la Bunge la Marekani la Capitol Hill na 'kuirejesha nchi yao nchi yao' wakati wabunge na maseneta wakiwa kwenye vikao vya kuhakiki na kupitisha ushindi wa Biden.

Katika uvamizi huu, mtu mmoja alipigwa risasi na kufariki huku askari polisi akijeruhiwa na kufa baadaye hospitalini mbali na wengine wanne waliofariki kutokana na kukosa huduma za matibabu. Wahuni hawa walijitokeza wakiwa na bendera ya kibaguzi na ya ile yenye maandishi ya Trump.

Baada ya shambulizi hili la aibu na hatari, maseneta na wabunge walirejea Capitol Hill na kumaliza kupitisha ushindi wa Biden.

Walivamia wakiwa chini ya uenyekiti wa Makamu wa Rais Pence huku usalama wake, familia yake na wabunge ukiwa hatarini.

Kituko ni kwamba, askari wa jiji la Washington na wengine wa vyombo vya usalama hawakuonekana kama walivyofanya wakati wa maandamano ya amani ya watu weusi ya Black Lives Matter kabla ambapo walijazana na kuwasambaratisha kwa mabomu ya machozi na pilipili na risasi za mpira.

Hili licha ya kuonyesha ubaguzi wa kimfumo limewaacha wachambuzi wengi hoi. Baada ya kwisha kwa kadhia hii, hadi makala hii inaandikwa, Trump hakuwa amewasiliana na Pence ambaye waandamanaji walikuwa wakisema anyongwe kwa kumsaliti mpendwa na kiongozi wao Trump.

Je, ilikuwaje Trump akawahadaa Wamarekani kiasi cha kupata umaarufu na nguvu hivi? Profesa Makau Mutua anasema kuwa watu wanapenda sana kusema na kusikia uongo (Daily Nation, 10 Januari, 2021). Hivyo, msidhani ni waswahili tu wanaohadaiwa na kuchezewa na wanasiasa bali hata watasha. Binadamu ni binadamu tu.

Baada ya Trump kuchochea kile ambacho wachambuzi hata viongozi wengi wa Marekani, akiwamo Rais Mteule Biden, walikiita jaribio la mapinduzi, maasi, ugaidi wa ndani, ujambazi, uhuni na kila aina ya majina, wapo wanaodhani kuwa ni wakati mwafaka kumtimua Trump toka madarakani hata kama amebakiza siku chache muda wake kikatiba kuisha.

Kitendo cha Trump, licha ya kutia aibu taifa la Marekani, kimefichua uozo wa kimfumo ambao ulimwezesha mtu anayesifika kwa uongo na majigambo kuchaguliwa kuwa rais wakati alionyesha wazi kutofaa kuongoza hata mkoa achia mbali nchi. Wengi walidanganywa na utajiri wake wa kutia shaka na uongo.

Chanzo kikuu cha Trump kufanya machukizo na makufuru ni kupinga kushindwa katika uchaguzi aliosema uliibiwa ilhali serikali yake ndiyo iliyouandaa na kusimamia.

Katika kupinga ushindi wa Biden, Trump alifungua kesi zaidi ya 60 mahakamani na kushindwa zote tena nyingine zikisikilizwa na majaji aliowateua mwenyewe.

Kwa mara ya kwanza, Rais wa Marekani aliamua kushambulia taasisi muhimu ya kidemokrasia yaani mhimili mmojawapo wa dola. Kitendo kilichowaudhi na kuwadhalilisha wamarekani kiasi cha kuona kama ule ushafaa wao duniani kuhatarishwa na mtu ambaye alihadaa wakamchagua kulinda taasisi husika akaishia kuzishambulia na kuzidhalilisha.

Rejea kuendelea kuendeshwa na mfumo wa kibaguzi ambao uliwadhalilisha watu weusi hadi miaka ya 70. Rejea ubaguzi wa chini chini wa kimfumo unaoendelea kwenye taifa hili sawa takribani karibu nchi zote za kimagharibi. Ukiishi kwa upanga, unakufa kwa upanga, wahenga walinena.

Trump, mfanyabiashara mwenye kutia shaka amefanikisha kitu kimoja, yaani kuufichua na kuutumia udhaifu wa kimfumo kuiadabisha Marekani kiasi cha kuumbuka tena ndani ya saa 24. Kama ni kipigo, hiki ni kikubwa cha muda mfupi kuwahi kulikumba taifa lolote.

Hakika, tarehe 6 Januari, 2021 ibaki kuwa siku ambayo Marekani ilivuliwa nguo na kuhujumiwa na rais wake mwenyewe.

Ama kweli mjenga na mbomoa nchi ni mwananchi mwenyewe saa nyingine anaweza kuwa rais wake kama ilivyotokea Marekani.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

# Chonde chonde viongozi staha muhimu

**Someni Kwa Furaha, na vingine vingi kama vya Alfu Lela Ulela, Mashimo ya Mfalme Suleiman na Hadithi za Adili na Nduguze. Tukirudi kwa simulizi ya Kalumekenge, tunajifunza jinsi lazima inavyoweza kutumika katika kuhakikisha jambo linafanyika. Amri inavyoweza kutumika kufikiwa jambo.**

MNAOKUMBUKA simulizi za zamani, hamtanisahihisha nikikumbuka ile ya Kalumekenge aliyekataa kwenda shule, ikabidi aombwe mbwa amng'ate, ili aende shule.

Mbwa alipokataa kumng'ata Kalumekenge, fimbo aliambiwa ampige mbwa ili amng'ate Kalumekenge na Kalumekenge aende shule. Lakini fimbo naye alikataa kutii amri ile.

Hivyo akaambiwa moto amuunguze fimbo, aliyekataa kumpiga mbwa aliyekataa kumng'ata Kalumekenge, aliyekataa kwenda shule.

Moto alipokataa kumuunguza fimbo aliyekataa kumpiga mbwa aliyekataa kumng'ata Kalumekenge aliyekataa kwenda shule, maji aliombwa amzime moto aliyekataa kumuunguza fimbo, aliyekataa kumpiga mbwa, aliyekataa kumng'ata Kalumekenge aliyekataa kwenda shule.

Tofauti na waliomtangulia, maji alikwenda kumzima moto, naye akaenda kumuunguza fimbo, fimbo akampiga mbwa naye akamng'ata Kalumekenge na hatimaye akaenda shule.

Hizi ni baadhi ya simulizi zilizokuwa na mafunzo kwa jamii kupitia kwa wanafunzi waliokuwa wakisoma vitabu jamii ya Someni Kwa Furaha, na vingine vingi kama vya Alfu Lela Ulela, Mashimo ya Mfalme Suleiman na Hadithi za Adili na Nduguze.

Tukirudi kwa simulizi ya Kalumekenge, tunajifunza jinsi lazima inavyoweza kutumika katika kuhakikisha jambo linafanyika. Amri inavyoweza kutumika kufikiwa jambo.

Nenda, ng'ata, piga, unguza, zima! Hizo ni amri zilizotumika katika sakata hilo la Kalumekenge na dhana nzima ya kwenda shule. Maana yake, Kalumekenge hakuwa anataka shule, lakini nguvu zilitumika hatimaye akaenda.

Hata waliosaidia mpaka Kalumekenge akaenda shule, nao walilazimishwa kufanya hivyo tena kwa vitisho. Kifupi hakukuwa na hiari, hakukuwa na kubembelezana, wala hakukuwa na mazungumzo ya kuleta maridhiano. Lakini hatimaye azma ilifikiwa.

Enzi za vitabu hivyo, zilikuwa za muda mfupi baada ya Wakoloni kuziacha nchi zetu za Afrika, hivyo katika kujenga mataifa mapya, kulikuwa na kusukumana hapa na pale. Pengine elimu ya maneno haikutosha bila mabavu kutumika.

Je, baada ya mataifa haya kupata uhuru, bado kuna haja ya kutumiwa mabavu mtu kwenda kupata jambo jema? Hivi kuna kulazimishana kwenda shule? Kina Kalumekenge bado wapo katika jamii zetu? Bila shaka hapana, kila mtu anajua wajibu, nafasi na fursa aliyonayo katika kujikomboa kama yeye na Taifa lake.

Kama ndivyo, inashangaza kuona wapo watu tena viongozi, wanaodhani kuwa kuna wenzao wana fikra kama za kina Kalumekenge, kwamba bila kusukumwa au kutishwa, hawawezi kufanya kazi.

Naamini tunakosea sana kufikiria hivyo, kwani si nadra siku hizi, kushuhudia kiongozi akimkaripia kiongozi mwenzake hadharani tena mbele ya wadogo zake kikazi, kwa sababu tu kuna jambo halikufanyika inavyotarajiwa.

Utashangaa bila hata kuulizia sababu, kiongozi atafokewa kama mtoto mdogo bila staha, na kujiona mtu asiyestahili kuwa na nafsi aliyonayo. Ilipata kushuhudiwa, Disii akimfokea Mkurugenzi wake hadharani, kisa kuchelewa kufika eneo la tukio.

Ilipata kushuhudiwa Waziri akimfokea hadharani, Mkuu wa chombo cha usalama nchini, kisa kuchelewa tena dakika tano, kufika eneo la tukio na hata kumtimua eneo hilo, bila hata kutaka kusikia kilichomsibu kabla!

Tunasikia sasa wakuu mbalimbali wakitisha wadogo zao wa kazi kuwaweka ndani na hata pengine kuamuru wawekwe ndani, kwa sababu tu kuna jambo limeonekana na mushkeli. Yanafanywa haya bila upande wa pili kusikilizwa na hata ukisikilizwa, hauaminiki!

Hii inafanyika, bila hata kujali tofauti za umri wa mtoa amri na mpokea amri, kwamba hata kama kuna makosa, kuna namna ya kumwambia kaka huyu au dada huyu, au baba au mama, au shangazi au mjomba huyu mbele za watu.

Mbona kuna nyakati Mkuu wa Nchi huonesha staha anapokuwa hata akitaka kumrudi mtu anayemzidi umri? Licha ya kuwa hivyo, lakini kuna wakati hujifikiria kuwa kiumri ni mdogo, hivyo hutafuta jinsi ya kufikisha ujumbe wake. Hatumii ng'ata, piga, unguza au zima. Anatumia saikolojia ya ualimu alionao.

Kwa kawaida, mwalimu akiwa mkali, hata somo lake inakuwa vigumu kueleweka kwa wanafunzi, kwa sababu hulifanya kwa kujilazimisha na kwa hofu kubwa, hivyo viongozi tutumie njia za staha kukosoana na hata kukaripiana, si lazima hadharani, kuna ofisi na kuna faragha. Alamsiki!

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Watendaji kichefuchefu mamlaka za maji watumbuliwe tupate huduma



Na Thobias Mwanakatwe

**Naibu Waziri wa Maji pia akiwa mkoani Songwe alishangazwa kuona wananchi katika miji ya Vwawa na Mlowo wakitozwa bili ya maji ya Sh. 20,000 na zaidi kwa mwezi huku taasisi kama Magereza na Polisi zenye watumiaji wa maji zaidi ya 70 zikitozwa bili ya Sh. 3,000 kwa mwezi.**

MWEZI Machi kila mwaka, Tanzania huungana na mataifa mengine kwa ajili kusherehekea maadhimisho ya wiki ya maji.

Hapa kwetu, Wizara ya Maji ndiyo imekuwa ikiratibu Wiki ya Maji kitaifa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa sekta ya maji.

Maadhimisho haya ambayo yalianza kuadhimishwa mwaka 1993, yanatokana na Azimio Na. 47/193 la Umoja wa Mataifa (UN) kuwa kila ifikapo Machi 22 ya kila mwaka nchi wanachama ziadhimishe Siku ya Maji Duniani kwa pamoja.

Hii ni Katika kutambua umuhimu na thamani ya maji kwa maisha ya binadamu na uchumi wa dunia kwa ujumla.

Lengo kuu la maadhimisho ya Wiki ya Maji nchini ni kuungana na mataifa mengine kutathimni utekelezaji, mafanikio, changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya maji na kuainisha mikakati ya kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira na kusimamia utunzaji wa rasilimali ya maji nchini.

Tangu mwishoni mwa mwaka jana 2020, tumeshuhudia na tuendelea kushuhudia Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na Naibu wake Maryprisca Mahundi, wakifanya ziara mikoani kwa kasi kukagua miradi mbalimbali ya maji inayotekelezwa na iliyokwisha tekelezwa.

Mawaziri hao katika ziara zao wamekuwa wakikumbana na vituko vingi kutokana na baadhi ya miradi iliyojengwa kutotoa maji huku serikali ikiwa imekwishatoa mamilioni ya fedha kuijenga.

Kwa kutaja mifano michache tu Naibu Waziri wa Maji alipofanya ziara wilayani Mbarali, mkoani Mbeya na kutembelea mradi wa maji Uhamila, akiwa na viongozi wengine akiwamo diwani, Meneja wa Mamlaka ya Maji Ludewa, hakuwapo eneo la mradi na hivyo alipigiwa simu na waziri kuulizwa kama mradi huo unatoa maji.

Pengine bila kujua kwamba anaongea na waziri akiwa eneo la tukio, alijibu kuwa mradi huo unatoa maji kila siku kwa wananchi.

Baada ya kubanwa kwa maswali na waziri, meneja akatoa sababu ya kutotoka maji kuwa ni tatizo la 'low voltage' ya umeme na sababu nyingine ni kwamba kwa muda mrefu hayuko Mbarali yuko wilayani Musoma kumuuguza mama yake ambaye anaumwa kichaa.

Naibu Waziri wa Maji pia akiwa mkoani Songwe alishangazwa kuona wananchi katika miji ya Vwawa na Mlowo wakitozwa bili ya maji ya Sh. 20,000 na zaidi kwa mwezi huku taasisi kama Magereza na Polisi zenye watumiaji wa maji zaidi ya 70 zikitozwa bili ya Sh. 3,000 kwa mwezi.

Kwa upande wake Waziri wa Maji, Aweso katika ziara zake mikoani amekuwa akichukua hatua kadhaa ikiwamo kumtumbua kazi Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Dodoma.

Serikali imekuwa ikipeleka mamilioni ya fedha kwa ajili kujenga miradi ya maji, lakini cha kushangaza ipo inayojengwa na haitoi maji jambo ambalo linasikitisha kwa wataalam hawa wa maji ambao kila mwezi wanakinga mikono kupokea mishahara inayotokana na kodi za wananchi.

Watendaji wazembe katika Mamlaka za Maji kwa kiwango kikubwa ndio wanasababisha kero ya maji iendelee kuwapo nchini na kusababisha tatizo hili kuwa kilio cha nchi nzima kwa wananchi.

Uzembe huu wa watendaji sasa ifike mwisho kwa mawaziri kuwachukulia hatua wataalam wa idara za maji wazembe, maana waswahili wanasema ukicheza na nyani utavuna mabua.

Haiwezekani tangu nchi ipate Uhuru mwaka 1961 bado kuna baadhi ya maeneo wananchi hawapati maji na si kwa sababu kwamba serikali haitoi fedha, ila utekelezaji wa miradi unakwamishwa na baadhi watendaji wazembe katika mamlaka za maji kwa kushindwa kusimamia vizuri miradi.

Nilifurahishwa na kauli ya Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso alipotembelea mradi mkubwa wa maji katika Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Alisema kilele cha maadhimisho ya wiki ya maji nchini mwaka huu kitatoa hatima ya baadhi ya viongozi na watendaji wa Mamlaka za Maji na wakala za maji vijiji (RUWASA) ambao watashindwa kukamilisha miradi kichefuchefu ambayo imekaa muda mrefu bila kukamilika.

Mimi nichukue nafasi hii kuwapongea Waziri wa Maji na Naibu Waziri wa Maji kwa kasi ya kushughulikia kero ya maji waliyoianza hivyo kinachotakiwa ni sisi wananchi kuwapa ushirikiano ili azma ya kusambaza maji nchi nzima iweze kufanikiwa.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI WIZARA YA MAJI**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com au WhatsApp 0762-183666.**

## DARASA LA NDOA

# Fahamu majukumu ya baba kwa watoto



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Baba anao wajibu wa kuwafundisha watoto wake, kuweka kanuni na kutoa mwelekeo wa familia yake. Katika kutimiza wajibu huu, baba anapaswa kuwa na muda wa kuzungumza na kuwasikiliza watoto wake ili kujua wanawaza nini, changamoto walizonazo, na mitazamo yao kuhusu maisha ili aweze kuwarekebisha na kuelekeza.**

BABA ni msingi na kioo cha familia. Msingi ukiwa imara, nyumba itakuwa imara, msingi ukiwa dhaifu nyumba itabomoka kirahisi. Tunaishi katika jamii inayobadilika kwa kasi na tunashuhudia kesi nyingi kuhusu kinababa wasiowajibika katika familia zao. Majukumu mengi katika familia wameachiwa wanawake.

Vijana wengi wanaooa leo, wameshindwa kuwa baba wazuri katika familia zao. Wengi wao hawajitambui wao kuwa ni nani na hawajui wajibu wao katika familia kuwa ni upi. Moja ya sababu zinazochangia katika tatizo hili ni makuzi wakati wa utoto. Wengi wao wana uzoefu mbaya kutoka kwa baba zao.

Baba alikuwa hatimizi majukumu yake kwa familia; haonekani nyumbani na wala haimsumbui kutokuonekana nyumbani; hana muda na watoto wake; wengine wana uzoefu wa mama yao kupigwa na baba yao; hawajawahi kuona matendo ya upendo ya baba kwa mama yao. Baba amekosa kuwa kielelezo kizuri kwa watoto wake.

Matokeo yake nao wanafanya vivyo hivyo kwani ndicho walichokiona na kujifunza kutoka kwa baba zao. Wanakuwa watu wasiojali familia kwani ndivyo walivyotengenezwa. Wengine ni wakatili kwa wake zao kwa sababu baba zao walikuwa wakatili kwa mama zao. Tabia fulani zinakuwa zimehamishiwa kwao na kuamini kuwa huo ndio mtindo wa maisha. Hali hii imesababisha matatizo mengi katika ndoa nyingi za leo.

Kuwa baba ni jukumu kubwa. Kwa hiyo ni muhimu sana wababa wafahamu majukumu waliyonayo kwa watoto wao ili kujenga familia bora. Yafuatayo ni majukumu ya baba kwa watoto wake:

**KUMPENDA MAMA YAO**

Baba anao wajibu wa kumpenda mke wake. Upendo huo huleta bubujiko la furaha kwa familia nzima. Watoto wanajifunza jambo jema ambalo linaweka msingi wa kupenda wanadamu wengine katika maisha yao. Kinababa wengi wameshindwa kuwafundisha watoto wao upendo kwa vitendo.

Matokeo yake watoto wanakosa upendo kwa sababu hawakukuzwa hivyo. Baba asiyempenda mke wake anatengeneza mazingira ya kuchukiwa na watoto wake, kwani mama anayo nguvu kubwa ya ushawishi na hamasa kwa watoto kuliko baba.

**KUFUNZA**

Baba anao wajibu wa kuwafundisha watoto wake, kuweka kanuni na kutoa mwelekeo wa familia yake. Katika kutimiza wajibu huu, baba anapaswa kuwa na muda wa kuzungumza na kuwasikiliza watoto wake ili kujua wanawaza nini, changamoto walizonazo, na mitazamo yao kuhusu maisha ili aweze kuwarekebisha na kuelekeza. Kufunza ni sehemu ya kuwasaidia watoto kujitambua.

**KUJENGA NIDHAMU**

Baba amepewa na Mungu misuli ya kuwekeza nidhamu kwa watoto wake, hivyo, mtoto/watoto wanapokosa nidhamu, mtu wa kwanza wa kulaumiwa ni baba, na siyo mama. Kwa sababu baba anayo mamlaka na nafasi kubwa ya kumrekebisha mtoto na kumtengeneza kuwa na nidhamu bora.

Kujenga nidhamu ya mtoto au watoto si jukumu la mama, bali ni jukumu la msingi la baba. Mama yupo kumsaidia baba kutimiza majukumu yake ipasavyo.

**KUONYA**

Baba ana wajibu wa kuadibisha watoto wake ili wakue katika kimo na maarifa; wampendeze Mungu na wanadamu. Watoto watahadharishwe kuhusu mambo yanayoweza kuwapoteza, kuwaharibu na kuvuruga mstakabali mzima wa maisha yao.

**KUTOA MIONGOZO**

Baba anao wajibu wa kutoa miongozo ya maisha kwa watoto wake; kuwatia moyo kwani kuna wakati watoto wanakutana na mambo yanayowachanganya akili na kuwakatisha tamaa.

**KUTUNZA**

Kinachomfanya mtu aitwe baba ni majukumu aliyoyabeba katika familia yake na si mtoto au watoto alionao. Watoto wasipotunzwa, mtu anapoteza sifa na thamani ya kuwa baba. Anabaki na sifa ya kuwa mwanamume tu.

Baba wa kweli atatunza watoto wake. Mungu anatupa zawadi ya watoto ili watunzwe. Kutunza maana yake ni kuwapatia watoto mahitaji yao ya msingi na kuwa na muda nao. Kwa asili wababa wanayo majukumu mengi. Hata hivyo, majukumu yasiwe kisingizio cha kudumu cha kukosa muda na watoto.

Kwa ujumla, malezi ya watoto ni jukumu la baba na mama. Mama na baba kila mmoja ana nafasi na wajibu katika familia. Katika makala hii tumejikita zaidi kwa baba kwa sababu baba ni msingi na kiongozi wa familia.

Kuwa baba ni jukumu kubwa. Baba mzuri ni yule anayetambua majukumu yake na anayejitambua kuwa yeye ni nani. Baba asipotimiza wajibu wake, anawakosesha watoto wake mambo mengi na kuifanya familia yake kukosa mwelekeo mzuri.

Baba anapotimiza majukumu yake anaweka msingi imara wa nidhamu na maadili mema kwa watoto. Nidhamu na maadili mema hujengwa pale baba anapompenda mke wake, anaposikiliza watoto wake, anapowatunza, anapowafunza, anapowaonya, anapowarekebisha, anapowaadibisha, anapoweka kanuni na miongozo mbalimbali ya kusimamia familia ili kujenga familia imara.

Yote haya yatawezekana kama baba atakuwa na muda na familia yake. Baba anapotimiza majukumu yake kwa watoto anaongeza na kutunza thamani, mamlaka, na nafasi yake kwa watoto wake.

**●Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.**

# MAISHA

JANUARI 17, 2021
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 10


**Ni mtoto wako lakini unazijua tabia zake?**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

ondoo jinsi ya kupamba
yumba mitindo maarufu



**HARUSI**

Ukurasa 12



**SHINGO YA TWIGA**

## Maziwa mtindi, limao inatosha kuitengeneza

Ukurasa 14

# Ni mtoto wako lakini unazijua tabia zake?

**Na Moses Ismail**

NI mtoto wako haswa! Hana mzazi mwingine zaidi ya wewe na mama yake au wewe na baba yake. Ni mtoto wenu na hilo halina shaka kabisa!

Tangu azaliwe mpaka anafikisha umri wa miaka tisa sasa, mmemlea nyinyi wenyewe, hajawahi kulelewa na watu wengine, iwe bibi na babu yake au shangaza na mjomba. Hujawahi kulelewa kabisa na watu wengine.

Kwa umri alionao unaamini kwamba unamfahamu sana, unaamini unajua anachokipenda na asichokipenda na hata wakati mwingine wakati wa 'stori' na marafiki zako pale mnapo ongelea watoto wenu, unazungumzia tabia zake.

Lakini ukweli wa mambo ni kuwa tabia hizo unazo zungumzia mbele ya wenzako, juu ya mwanao, si tabia zake halisi za sasa, mwanao hayupo hivyo kabisa. Humjui wala hujui lolote lile kuhusu tabia zake halisi.



Tabia hizo unazozungumzia leo, ni tabia zake za miaka minne mitano iliyopita, wakati ule ulipokuwa na nafasi ya kuwa naye na kuzungumza naye mawili matatu kama baba na mtoto na pia kupima uwezo wa ufahamu wake.

Tabia zake chache za sasa unazo zingumzia, ambazo ni za sasa, ni zile tu unazoziona mara moja moja unapopata nafasi ya kukaa naye sebuleni na pengine kwa usumbufu anaokupa kwa kutaka kitu hiki na kile.

Kwa mfano, unajua anapenda kucheza mpira kwa sababu kila wakati anakuomba umnunulie vifaa vya mpira kama viatu na jezi ama unajua pia kuwa anapenda kuchora kwa sababu hiyo hiyo, ya kutaka umnunulie vifaa.

Ni kweli kabisa, mtoto wako anapenda kucheza mpira na anapenda pia uchoraji na uko sahihi kabisa kwa kusema hivyo. Ila, unajua ni nafasi gani anacheza kwenye mchezo huo na ana uwezo gani wa uchoraji?

Umeshawahi kuona michoro yake au umeshawahi kushiriki katika mechi moja ya mpira wa miguu anayocheza na kumtia moyo au kumshauri ili afikie mafanikio makubwa zaidi katika mmoja ya jambo hilo analopenda?

Ukweli ni kuwa hujawahi kufanya hivyo hata siku moja kwa sababu nafasi yako ya kufuatilia mambo yake ya kitoto ni ndogo sana na wala huoni umuhimu wa kufanya hivyo. Utapata wapi muda huo?

Mpira na uchoraji ni mifano tu, ila kiuhalisia watoto wana tabia nyingi ambazo pamoja na wazazi kujifanya kuwa wanazijua, ukweli ni kuwa hawazijui kama inavyopaswa kuzijua. Hawana muda wa kukaa nao.

Utaijua vipi tabia za mwanao, ambazo ndizo taswira halisi inayomuonyesha yeye ni nani, wakati huna muda kukaa naye na kuongea naye kirafiki kwa kisizingio cha kukosa muda? Utazijuaje?

Kupotoka au kutengamaa kwa tabia za mtoto kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na wazazi kukosa kuwapa watoto muda wa kushiriki kwenye michezo au mazungumzo nao vitu vikubwa vinavyomjenga mtoto kitabia.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**Comment t'appelles – tu?: Unaitwa nani?**

1. Soma dayolojia ifuatayo katika lugha ya Kifaransa na ujaze sehemu zilizokuwa wazi.

Dayolojia

Katika lango kuu la kuingia katika Shule ya Sekondari, baada ya likizo ya masomo kuisha, Raswiina na Sarah wanakutana na marafiki wapya.

**Raswiina:** Salut!
**Sarah:** Salut!
**Raswiina:** Comment vas – tu?
**Sarah:** Je vais bien, merci. Et toi?
Raswiina: Je vais bien egalement.
**Sarah:** Comment t'appelles – tu?
Raswiina: Je m'appelle Raswiina.
**Sarah:** Moi, c'est Sarah. Je suis de Dodoma. Raswiina: Je suis ravi de te connaitre, Sarah.
**Sarah:** Moi de meme.
**Sarah:** Quel est le nom de ta copine?
**Raswiina:** Elle s'appelle Mariam. Elle vient de Kilimandjaro comme moi!
**Sarah:** Salut Mariam, je suis contente de faire ta connaissance!
**Mariam:** Je suis contente egalement de te connaitre, tu es sympathique!
Sarah anamuita rafiki yake mmoja wa darasani ambaye anakuja akikimbia.
**Sarah:** Je vous presente ma meilleure amie. Elle s'appelle Nathalie. Elle est francaise d'origine espagnole. Elle est en Tanzanie pour une annee. Elle habite dans ma famille. On est dans la meme classe.
Mariam et Raswiina: Nous sommes enchantees de faire ta connaissance, Nathalie! Nous te souhaitons la bienvenue dans notre lycee!
**Nathalie:** Moi aussi je suis heureuse de vous connaitre, vous etes tres gentilles!

**Maelezo ya kuzingatia**
**Jinsi ya kuuliza jina la mtu**


• Commenttut'appelles?–Unaitwanani (informal).
• Commentest–cequetut'appelles?–Hivi unaitwa nani? (informal).
• Commentvousappelez–vous?–Unaitwanani? (formal).
• Commentt'appelles–tu?–Unaitwanani? (informal).
• Comments'appelle–t–il?–Yeye(wakiume) anaitwa nani?
• Comments'appelle–t–elle?–Yeye(wakike) anaitwa nani?
• Quelesttonnom?–Jinalakoninani?(informal).
• Quelestsonnom?–Jinalakeninani?
• Quies–tu?–Weweninani?(informal).
• Quiest–elle?–Yeye(wakike)ninani?
• Quiest–ce?–Huyuninani?

Jinsi ya kujibu (ukiulizwa unaitwa nani).

! Je m'appelle Nathalie – Naitwa Nathalie.
! Il s'appelle Idd – Yeye (wa kiume) anaitwa Idd.
! Elle s'appelle Sulayhat – Yeye (wa kike) anaitwa Sulayhat.
! Mon nom est Beatrice (ou mon nom, c'est Beatrice) – Jina langu ni Beatrice.
! Son nom est John (son nom, c'est John) – Jina lake ni John.
! Moi, c'est Yusuph; elle, c'est Fadhila – Mimi ni Yusuph; yeye (wa kike), ni Fadhila.
! Je suis Benjamin – Mimi ni Benjamin. Jinsi ya kumtambulisha mtu.
"Je vous presente Monsieur Dupont, notre voisin – Na(ku/wa)tambulisha Bwana Dupont, jirani (wa kiume) yetu.
"Je te presente notre directrice – Nakutambulisha Mkurugenzi wetu (wa kike).
"Je te presente mes amis: Farida, Erick et Mariam – Nakutambulisha marafiki zangu: Farida, Erick na Mariam.
"Voici mon ami, Ben, il est ingenieur en informatique – Huyu ni rafiki yangu Beni, yeye ni mtaalam wa kompyuta.

## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

MAMA mmoja alikuwa anafanya usafi chumbani, ghafla aliona kisanduku chini ya uvungu wa kitanda. Alipokifungua alikuta kuna mayai 5 na Sh. milioni moja. Aliporudi mume wake alianza kumuhoji.

**MKE:** Kisanduku hiki cha nini?
**MUME:** Kweli unataka kujua?
**MMKE:** Ndio, kwani siku hizi tunafichana!!
**MUME:** Huwa nakwenda nyumba ya jirani kuiba mayai kila siku
**MKE:** Afadhali nimegundua mapema uache tabia hii. Hizi pesa je?
**MUME**: Huwa mayai yakijaa nayauza, kwa sasa yapo haya matano tu.
**MKE:** Tobaa!

SWALI
Bonde la mto Rufji ni maarufu kwa kilimo gani cha nafaka?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Napenda niitwe baba wa familia, vituko vya mke wangu kiwazo!

KARIBU tena msomaji wangu katika safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita tuliona kijana ambaye wazazi wa mchumba walimkataa, kisa anatoka familia yenye uwezo mdogo kiuchumi na pia elimu yake. Hata hivyo alimpata mwingine wa ndoto zake.

Wakati wengine wana shauku ya kuoa, wengine tayari kero zimewakifu wanatamani wazikimbie nyumba zao. Hakika Maisha Ndivyo Yalivyo.

Leo tuone kilio cha kijana mwingine aliyechoshwa na tabia za mke wake. Anasema ni kama mchezo wa kuigiza kwa yale anayopitia hadi anakata tamaa ya kuitwa baba wa familia. Kabla sijadadavua. Hebu tumsikie asemavyo katika ujumbe wake mfupi kupitia simu ya kiganjani. Anasema;-

"Anti hebu nisaidie, nina mwelekeo wa kukata tamaa ya kuishi na mwanamke maishani. Nina watoto wawili ila miaka yote hiyo nimekuwa wa kubembeleza maisha. Hebu fikiria simu ya mwanamke wangu hukaa sandukuni aki-chat na wanaume wengine kwa kificho. Je, nina mke hapo? Ni vituko hapana mfano.

Kingine hawapikiwi hadi saa sita au saba usiku. Mlo wa mchana watoto wanakula kati ya saa tisa hadi kumi. Ukimuuliza anakimbilia kwao hata kama ni usiku. Nikikaa na kufikiria sina picha ya kuishi na huyu mwanamke.

Kwa sasa ameanza tabia ya kuondoka bila kuaga. Napenda kuitwa baba wa familia, lakini sasa nimechoka. Sina moyo mkubwa tena nipate angalau furaha kidogo. Barikiwa kwa ushauri. Mengine ni mengi niishie hapa". Hivi ndivyo anavyohitimisha mpendwa wetu huyu.

Mpenzi msomaji wangu, bila shaka umesikia magumu yaliyosheheni changamoto anayopitia ndugu yetu huyu. Hata kuvumilia yote hayo, ni roho ya subira aliyoumbiwa ndani yake. Anaamini kuwa ipo siku atapata ufumbuzi.

Nami nichangie hapo kidogo niseme hivi;- Upo wakati tunapitia vita na majaribu makubwa yanayochoma mioyo yetu. Majaribu mengine yanatuumiza na kutuchosha.

Lakini neno moja unalopaswa kufahamu ni kwamba majaribu au vita tunavyopitia katika maisha vina uwezo mkubwa wa kutufundisha uvumilivu na ustahimilivu kuliko kitu kingine chochote.

Kila mtu ana miaka ya giza, kila mtu ana miaka ya kupita jangwani. Nikwambie msomaji wangu, ni katika miaka hii ya jangwani, ndipo nguvu, uvumilivu na ustahimilivu wako hupimwa. Na huwezi kujua kama una uvumilivu kama hujapitia miaka ya jangwani. Maisha ya jangwani nina maanisha misukosuko, mateso, majaribu, magonjwa na kadhalika.

Na wakati unapita kwenye jangwa hutagundua nguvu uliyonayo hadi utakapotoka huko jangwani. Yupo atakayeingia hatoki (hana nguvu), mwingine anaingia anatoka, huyu ana nguvu. Na ukishavumilia na kustahimili wakati huo, utashangaa vile Mungu atakavyokuinua na kukupelekea viwango vingine vya maisha yako.

Msomaji wangu, kijana niliyemzungumzia kwenye makala haya, ameeleza yale yanayoumiza moyo wake. Amekaa nayo akaona ayaseme apate ushauri kumfariji. Nimejaribu hapo juu kumtia moyo kwamba hayo ni majaribu, anapita jangwani, hivyo anapaswa kutafuta nguvu ya kumvusha. Kwani wakati mwingine kulalamika hakuwezi kutoa jawabu.

Lazima ajiulize, chanzo cha mkewe kufanya hayo yote kinatokana na nini? Je, utoshelezi ndani ya nyumba upo? Mahitaji yote muhimu ndani ya nyumba yapo? Inawezekana wakati mwanamke huyo anaolewa alitarajia mambo kadhaa ambayo sasa hayaoni.

Au yawezekana mazingira ya mahusiano kabla ya kuoana yalionyesha dalili za bibie kuwa wa ku-chat ambayo ameiendeleza, ni mzururaji, tabia ambayo hajaiacha. Kama jamaa angechunguza kwa makini tabia za mkewe kabla ya kuoa, angeweza kubaini madhaifu hayo.

Wapo wanaume wanaooa wanawake kwa kutizama sura na siyo tabia. Matokeo yake wanakuja kuweka mikono kichwani eti 'laiti ningejua', kumbe ameshachelewa na sasa inabidi maji aliyoyavulia nguo ayaoge tu, hakuna namna.

Na pia kama alijitamkia 'kipenda roho hula nyama mbichi', hayo anayopitia leo ni matunda ya 'uamuzi pupa' wenye majuto! Maisha Ndivyo Yalivyo.

***Msomaji wangu, kwa leo niishie hapa. Hebu mpe ushauri kijana huyu kwa kuleta maoni yako au kisa cha kimaisha kupitia 0715268581. Namba hii pia ipo WhatsAPP***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Bei za vyakula kwa wasafiri ni maumivu, ziangaliwe

UNAPOSAFIRI kwenda mkoa wowote, kuna utaratibu wa mabasi kusimama kwenye hoteli au eneo lenye kutoa huduma ya chakula kwa abiria kununua chochote kwa ajili ya kula au kunywa.

Sehemu hizo mara nyingi huwa eneo la mjini au nje ya mji zenye huduma zote muhimu za kijamii kama choo, vyakula na mahitaji mengine muhimu kwa binadamu, lakini maumivu ya watumiaji ni makubwa kutokana na kutokuwa na mbadala.

Katika maeneo hayo hakuna bei elekezi ya huduma yoyote bali wauzaji hujiamulia tu jambo ambalo ni maumivu kwa abiria wenye vipato tofauti na hasa wa kipato cha chini ambao huamua kutokula chochote au wanavyojitayarishia kwa ajili ya safari mbavyo baadaye hupoa.

Mathalani, maji huuzwa mara mbili ya bei halisi ambayo tayari ina faida kwa muuzaji kiasi kwamba mwananchi wa kipato cha chini aliyekuwa na nauli ya kusafiri pekee anashindwa kununua.

Ukienda kwenye chakula ndiyo kabisa bei ni mara mbili hadi mara tatu, sahani moja huuzwa kati ya Sh.7,000 na 8,000 kiasi ambacho mtu wa kipato cha chini ambaye anatumia usafiri wa umma hawezi kumudu.

Aidha, chakula hicho huwa ilimradi tu ule kujaza tumbo kwa kuwa hakilingani na thamani ya fedha anayotoa mtu kukinunua na wakati mwingine vinakaa muda mrefu kwenye jokofu na kupoteza ladha.

Wakati mwingine havipikwi vikaiva vizuri, mfano ni viazi vinavyo tengenezwa chips, wengine huvimenya hadi vile vinavyoanza kuharibika kiasi cha kuonekana kama uchafu, lakini wanunuaji hawana namna na kulazimika kununua.

Mara kadhaa abiria hulalamikia bei hizo, lakini hakuna wa kusikiliza kilio hicho, jambo ambalo sio sahihi. Cha kujiuliza ni kwamba bei inapangwa na nani? Na aliyepanga alitumia vigezo gani au kwasababu ni hoteli ya wasafiri?

Mbaya zaidi abiria hana uamuzi kwa kuwa basi husimama eneo fulani kutokana na matakwa ya dereva na wasaidizi wake, ambao wengi hawalipi huduma yoyote kwa kuwa ndiyo wamepeleka abiria wengi katika eneo husika.

Wakati mwingine huduma hizo zinapatikana maeneo ya mjini jambo linalozua maswali kuwa kwanini bei katika hoteli au eneo hilo ni tofauti na kwingine, nini kinafanya maji ya Sh. 500 yauzwe Sh.1,000? Au nini kinapandisha bei ya chakula kutoka Sh. 4,000 hadi 8,000 kwa chakula ambacho kwenye hoteli nyingi kina thamani ya Sh 3,000 hadi 4,000.

> **Au nini kinapandisha bei ya chakula kutoka Sh. 4,000 hadi 8,000 kwa chakula ambacho kwenye hoteli nyingi kina thamani ya Sh 3,000 hadi 4,000.**

Wakati mwingine abiria huuziwa nyama ambazo hazijaiva vizuri, zilizolala na zisizostahili kuliwa, lakini kwa sababu muda wa kula ni dakika 10 basi abiria hubeba ili ale ndani ya gari, lakini hushindwa kula na kukitupa kwa kuwa ni chakula kibaya kilichopikwa ilimradi bila kujali mlaji na thamani ya fedha.

Ni muhimu sana mamlaka za kiserikali zikaingilia kati suala hili na bei hizi hata kama ni soko huru, lakini lazima kuangalia namna watu wanavyovuna fedha kupitia safari za abiria.

Cha kushangaza hoteli nyingine zipo mjini na si kwamba gharama za kusafirisha bidhaa ni kubwa kiasi cha kuwafanya kuuza mara tatu hadi nne ya bei, lakini kwa kuwa tu chakula hicho kitaliwa na msafiri basi ni ghali.

Bila kufuatilia kwa kina abiria wanaumia na wachache wananufaika zaidi jambo ambalo halistahili kuwa hivyo, tunatarajia sasa halmashauri husika zifuatilie kwa kina kuona kinachotendeka na kama ndicho kilichopitishwa jamii ielezwe sababu za kuziruhusu hoteli hizo kuwaumiza abiria kwa kuuza bei mara mbili au tatu.

***Mungu ibariki Tanzania***

***Kwa maoni au ushauri: kitomari.salome@gmail.com***

# HARUSI



Ni ndoa **Joel John** na **Anna Luwoga**, Iliyofanyika Tanga, Januari 2, 2021



# MITINDO



NGUO NYEUSI

## Inang'arisha na kuficha uchafu

WATU wa aina zote wanatakiwa kuwa makini katika kufanya chaguo sahihi la mavazi ili waendane na mazingira ya kisasa.

Lakini kwa wanaume kutokana na tabia zao za kutojali sana kuchagua aina za mavazi, wanatakiwa kuwa na mavazi ambayo hayatawapa tabu wakati wanapovaa.

Kutokana na tatizo hilo wanajikuta wakivaa nguo ambazo hazikubaliki na hazilingani na mahitaji ya mwili wake.

Wataalamu wa masuala ya mavazi wanasema moja ya kanuni ya vazi ni mtu anatakiwa kuwa makini wakati wa kununua.

### JINSI YA KUCHAGUA

Watu wavivu wa kununua nguo au kufanya usafi, vazi la rangi nyeusi linakufaa kwa sababu zina kawaida ya kutochagua rangi wala kuchosha muonekano wa mtu.

Mwanamume anapovaa suruali yeusi haitaji kufikiria sana kuhusu rangi ya shati au kiatu.

Suruali nyeusi, inaendana na shati au fulana ya rangi yoyote yenye mng'aro na ukatoka bomba.


Unashauri kuchukua yenye kubana kiasi kwa sababu unapovaa na shati muonekano wako unakuwa wa kipekee.

### VIATU

Suruali nyeusi inafaa sana kuvaliwa na viatu vya rangi nyeusi, dongo au nyeupe iliyofifia.

Hata hivyo wengine wanapenda kuvalia viatu vya wazi vya rangi yenye mng'aro dhaifu na wanatoka bomba.

## UREMBO



Shingo ya Twiga

# Maziwa mtindi, limao inatosha kuitengeneza

JE, umesikia ule msemo unaosema 'Shingo ya Twiga' ambao unaelezea jinsi shingo ya mwanamke ambayo ina muonekano mzuri.

Kuwa na shingo nzuri ambayo haina mikato na rangi nyeusi, hufanya mwanamke kuonekana mrembo zaidi na anayejipenda.

Zipo sababu chache ambazo zinachangia mtu kuwa na shingo nyeusi na yenye mtazamo usiovutia

Wakati mwingine, tatizo hili linasababishwa na mkusanyiko wa uchafu ambao hufanya ngozi ya shingoni kuwa na rangi nyeusi na kukosa ulaini unaotakiwa.

Idadi kubwa ya shingo za wanawake zina asili ya mikunjo ambayo ngozi huhifadhi vumbi na chembe jasho shingoni kwa hiyo baada ya muda husababisha ngozi kuwa na rangi mbaya.

**MAZIWA YA MTINDI**

Ili kuondoa weusi huo, hakikisha unasafisha ngozi ya shingo kwa kutumia maziwa ya mtindi.

Unachotakiwa kufanya ni kujisugua shingoni kwa mchanganyiko wa maziwa ya mtindi na maji ya limao.

Pia unaweza kutumia sukari iliyochanganywa na mafuta ya mzaituni kama 'scrub' ya kujichua.

Jinsi ya kufanya kwa njia hizo zote mbili, ni kupaka shingoni baada ya kuwa imeoshwa kwa maji safi ya uvuguvugu.

Upakaji wake unatakiwa kuwa taratibu hadi unapohakikisha uchafu unatoka.

Lakini kumbuka kufanya hivyo nyakati za usiku tu ili kupata matokeo mazuri.

## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# ROSTI YA FIRIGISI





FIRIGISI ni aina ya kitoweo kinachopendwa na watu.

Kitoweo hiki hupikwa kwa njia ya kuchemshwa au kukaangwa.

Kwa sehemu kubwa migahawa ya chips huuza firigisi za kuku za kukaanga na maini yake.

Leo katika safu yetu ya mapishi tunaeleza namna ya kupika mboga ya firigisi ambayo inaweza kuliwa na wali, ugali au chakula chochote.

**MAHITAJI**

Firigisi nusu kilo, karoti moja, nyanya mbili, pilipili hoho ya kijani moja na pilipili hoho nyekundu moja.

Kitunguu maji kimoja, kitunguu saumu, tangawizi, chumvi

pilipili manga, giligilani ya unga, pilipili nyekundu, unga wa binzari nyembamba na ndimu.

**NAMNA YA KUPIKA**

Kwenye firigisi changanya chumvi, pilipili manga, pilipili nyekundu, unga wa binzari nyembamba, unga wa giligilani, tangawizi, vitunguu saumu na ndimu.

Weka mafuta kwenye sufuria kisha anza kukaanga firigisi zote pamoja mpaka ziive.

Katakata boga zote kisha weka kwenye firigisi, wacha mpaka nyanya ziive zilainike kisha mboga yako itakuwa tayari kwa kuliwa.

## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# Pendezesha kona ya chumba chako kubuni mapambo



KILA kona ya chumba iliyo tupu ni fursa yako kubuni namna ya kuipendezesha.

Wakati unaipendezesha una fursa ya kuitumia pia hata kama awali ilikuwa inaonekana haiwezi kufaa kwa matumizi.

Zipo njia nyingi za namna ya kubuni kutengeneza kona yako ikapendeza na hata kupendezesha nyumba yako pia.

Njia mojawapo unaweza kuamua ukaitumia kama shelfu ya kuhifadhia vitabu vyako kwa kuitengeneza kufuatisha muundo wa kona.

Hii ni moja ya njia nzuri za kufanya kona isiyokuwa na kitu itumike, na shelfu zinaweza kutengenezwa kwenda juu karibu ya dari kulingana na mahitaji na ukubwa wa kona.




Mbali na shelfu za vitabu, pia unaweza kutengeneza kona yako kwa ajili ya kuweka mapambo madogo. Kona hutumia kutengeneza sehemu ya kufanyia shughuli zako mbalimbali za kiofisi au kusomea.

Kumbuka sehemu ya kona ikitengenezwa vizuri ni nzuri zaidi na hutuliza akili hususani kwa wanaosoma.

Pia unaweza ukaitumia kona kama sehamu ya kutundika picha za familia.

Huhitaji ukuta mkubwa kwa ajili ya kusambaza picha za familia yako badala yake tumia kona hiyo kuongeza mvuto na pia usiweke nyingi zikakuharibia mvuto.

Unaweza kuweka ua la mmea wa kuoteshwa, shelfu au sanaa zozote na itasaidia kuingiza uoto asili ndani ya nyumba kwa sababu matawi yake yatatosha kuijaza kona yenyewe.

Kwenye chumba, kona hiyo unaweza kuitengeneza vizuri kama sehemu ya kutundikia nguo hasa cha kunyooshea nguo au kinachotumika kwa ajili ya kulala.

Hata katika chumba cha wageni ambacho mara nyingi huwa sio kikubwa, unaweza kuitumia kupachika hata mbao nyembamba inayoweza kukutanisha pande zote mbili za kuta na hapo ukatundika nguo zako na zikakaa katika muonekano mzuri.

Na kwa wenye sebule au vyumba vyenye nafasi ndogo, kona inafaa pia kuweka sofa hasa la duara lenye vipande viwili ambavyo vinaunganika.

Pia unaweza kupendezesha kona yako kwa kuweka vinyago ambavyo navyo lazima uweke juu ya meza ndogo au ukapatengenezea kabati au meza ya miguu mitatu.

Ni vizuri zaidi pia ukimtumia fundi kukufanya dizaini ya namna ya kutumia kona yako kulingana na kitu utakachoona kitaipendezesha zaidi.

## MPANGILIO

# Dondoo njinsi ya kupamba nyumba mitindo maarufu

**1.** Mtindo wa kisasa, mtindo huu ni kuwa na vitu vichache muhimu ambavyo kila kimoja kinatumika.


**2:** Mtindo wa saresare (classic)
Mtindo wa saresare unategemea mpangilio na uwiano.
Tabia kuu ya mtindo huu kuwe na kitovu cha upambaji kwa kugawa chumba pande mbili na kila kitu kwenye upande mmoja kinafanana.

**3:** Mtindo wa kiutamaduni, hapa fenicha na mapambo yana muonekano wa utamaduni wa watu fulani ila mapambo si mengi.

**4.** Mtindo mchanganyiko, mpambaji anachanganya mapambo kulingana na mitindo ya aina yote.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
NATAMANI NINGE-KUWA YUGANDA ALAFU NINGEKUWA 'MWANAMYUZIKI'
UNGEAMBULIA OFA' VILABUNI LAKINI SIO "URAIS"
NENDA KAIRUDIE 'KEMERA' NA TEPU REKODA!
UTAIFUATA WEWE ULIONG'ANG'ANIA TUKABALANSI KWA 'BOBU WAINI'
'AROOO! NYIYE!!!
YUGWANDA
'NISINGEPENDEZA?
HATA UKIGANDA JIKONI HUWEZI KUONA 'NITAKAVYOVINYUNYIZA' ILI USIBANDUKE KWANGU
SHINDWA!
TATIZO KATI YA ROHO NA KEMERA SIJUI NITETEE KIPI?
ULISIMAMA JUU YA JUKWAA UKASEMA WAVAA VIMINI SIO TAIPU YAKO...SASA MBONA LEO UNABWABWAJA?
KUUUMBEE! NDIO MAANA NAJIONA AKILI ZANGU NYEPESI
YALIKUWA MANENO YA KUOMBEA KURA... SI UNAJUA DOMO NI JUMBA LA MANENO!
NYIE WATU BADO MPO?...AU MPITA NJIA ULIYEPOTEA NJIA?
WATU GANI? HUU MWILI WA UGONJWA USTAKE KUNIJAZIA INZI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...KAMA SIO CHAKO ACHA KIKUPITE

## HABARI KIMATAIFA

### MATOKEO UCHAGUZI UGANDA:

# Museveni aongoza, Bobi Wine akidai ameshinda urais

**Kampala,** UGANDA

TUME ya Uchaguzi nchini Uganda, inaendelea kutangaza matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika Januari 14, mwaka huu, huku rais aliyeko madarakani, Yoweri Museveni akiongoza kwa asilimia 61.98.

Hiyo ni kwa mujibu wa matokeo yaliyotolewa usiku wa jana, wakati mpinzani mkuu wa Museveni, Robert Kyagulanyi, maarufu kama Bobi Wine, mgombea wa urais kwa tiketi ya chama cha NUP, akipata asilimia 30.91.

Aidha, Bob Wine alidai kushinda uchaguzi wa urais, dhidi ya Museveni, wakati matokeo yakiwa bado yanatangazwa na Tume ya Uchaguzi.

Tayari matokeo yaliyotengazwa na tume hiyo, yanaonesha kuwa Museveni, kiongozi wa muda mrefu nchini humo, anaongoza.

"Nina uhakika kuwa kumshinda Dikteta kwa mbali. Nawaomba Waganda wote kukataa udanganyifu.Tumeshinda uchaguzi huu, na tumeushinda kwa mbali," aliwaambia wanahabari akiwa nyumbani kwake jana.

"Kinachotangazwa ni wizi mtupu, tunayakataa."

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Jaji Simon Mugenyi Byabakama, alikanusha madai ya Bobi Wine.

Matokeo ya mwisho yalitarajiwa kutangazwa jana, jioni.

Wagombea wengine wa urais hawajafikisha hata asilimia tano ya kura, ambazo tayari zimehesabiwa.

Hata hivyo, matokeo ya ngome kuu za Bobi Wine maeneo ya mji mkuu, Kampala pamoja na wilaya jirani bado hayajatangazwa.

Matokeo rasmi ya uchaguzi wa urais yanatarajiwa kutolewa jioni, wakati makazi ya Bob Wine yakizingirwa na askari wa usalama na huduma ya mtandao wa intaneti zikiwa hazijarejea.

Bob Wine anaendelea kushikilia msimamo wake kuyapinga matokeo hayo, na tayari zaidi ya asilimia 86 ya kura zimekwishahesabiwa.

Museveni (76) anaongoza kwa kura 5,303,831 sawa na asilimia 58.83 huku mpinzani wake, Bobi Wine akiwa na kura 3,119,965 ikiwa ni asilimia 34.62 kwa mujibu wa Tume ya Uchaguzi Uganda.



Robert Kyagulanyi almaarufu Bobi Wine.

Mwenyekiti wa tume, Byabakama alisema kuwa upigaji kura ulikuwa kwa amani na kusifu mafanikio hayo.

Matokeo hayo yamekuwa yakitangazwa licha ya kuzimwa kwa mtandao, alisema :Hatutumii intaneti ya ndani ya nchi kutangaza matokeo. Tunatumia mifumo yetu wenyewe. Msiwe na hofu na matokeo licha ya kwamba hakuna intaneti," aliwaambia waandishi wa habari.

Bobi Wine, alisema baadhi ya wawakilishi wake katika vituo vya kuhesabia kura walikamatwa Alhamisi, na anaamini kuwa kuzimwa kwa intaneti kumetumika ili kuvuruga uhesabuji wa kura. Vilevile ni kama mawasiliano yote yamekuwa na shida kwa sababu watu wamekuwa na wakati mgumu kutuma ujumbe mfupi pia.

"Ningefurahi kuwashirikisha video za udanganyifu na kutofuatwa kwa utaratibu lakini mpaka intaneti irejeshwe," Reuters, ilimnukuu Bobi Wine.

**RFI/DW/BBC**

# EU yahofia kuwapo uhalifu wa kivita jimbo la Tigray

**Brusels,** UBELGIJI

UMOJA wa Ulaya (EU), umesema kuna uwezekano uhalifu wa kivita umefanyika kwenye jimbo la Kaskazini mwa Ethiopia, Tigray.

Mkuu wa Sera za Kigeni wa umoja huo, Joseph Borrell, alisema wamepokea taarifa za kuaminika kuhusu vurugu za kikabila, mauaji, uporaji mkubwa, ubakaji, kurudishwa kwa nguvu kwa wakimbizi na uwezakano wa uhalifu wa kivita.

Aidha, Borell aliwataka viongozi wa Ethiopia, kuruhusu kupatikana kwa msaada wa kibinadamu.

Zaidi ya watu milioni mbili ni wakimbizi wa ndani na wakati watu wanaohitaji msaada, na si rahisi kuyafikia maeneo yaliyoathirika kwa mapigano.

Hali hiyo inasababisha ugumu katika kutolewa kwa msaada wa kibinadamu.

Wakati huo huo, EU, umesitisha mpango wake kuisaidia bajeti ya Ethiopia wenye thamani ya euro milioni 88, hadi hapo mashirika ya kutoa misaada ya kibinadamu yatakaporuhusiwa kupeleka misaada Tigray kwa watu wenye uhitaji.

**DW**

# 30 wapoteza maisha, 15,000 wakosa makazi baada ya tetemeko la ardhi

**Sumawesi,** INDONESIA

HUKU nchi ya Indonesia ikiendelea kutafuta mabaki ya ajali ya ndege iliyobeba abiria 62, juzi waokoaji walifika katika tukio lingine kuwatafuta watu waliofukiwa na vifusi na kuua watu 30.

Wiki iliyopita, ndege iliyobeba abiria 62, aina ya Boeing 737 ya kampuni ya Sriwijaya Air, ilipoteza mawasiliano na rada dakika nne tu baada ya kuanza safari yake ya kuelekea eneo la Pontianak, Magharibi mwa Jimbo la Kalimantan.

Wiki hii, tetemeko lenye ukubwa wa richta 6.2, limetokea Ijumaa asubuhi na kusababisha mamia ya watu kujeruhiwa.

Maelfu ya watu wengine, hawana makazi yao baada ya tetemeko hilo kusababisha hasara katika kisiwa hicho.

Kisiwa cha Sulawesi kina historia ya kutokea kwa majanga ya tetemo la ardhi na tsunami mwaka 2018 watu zaidi ya 2000 walipoteza maisha baada ya majanga hayo mawili.

Mbali na makazi ya watu kuporomoka, majengo ya serikali ikiwemo hospitali, zimeporomoka pia.

Mwaka 2004, watu 226,000 walipoteza maisha katika kisiwa cha Sumatra baada kutokea kwa tetemeko la ardhi.

Uturuki ilichapisha ujumbe wa rambirambi kuwafariji wananchi na serikali ya Indonesia kufuatia vifo vilivyosababishwa na tetemeko la ardhi lililotokea nchini humo.

Katika taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje, iliandikwa,

"Tumepokea kwa masikitiko taarifa za kutokea kwa tetemeko la ardhi lenye ukubwa wa kipimo cha 6.2 katika mji wa Majene, Magharibi mwa Sulawesi nchini Indonesia, na kusababisha vifo vya watu wengi na majeruhi."

Taarifa iliambatana na ujumbe wa pole kwa serikali, wananchi wa Indonesia, ndugu, jamaa na marafiki wa watu waliopoteza maisha kwa kuwaombea Mwenyezi Mungu awarehemu, pamoja na kuwatakia afueni ya haraka majeruhi wote wa maafa hayo.

Mwenyekiti wa Wakala wa Maafa katika kanda ya Sulawesi Magharibi, Darno Majid, alitangaza idadi ya vifo iliongezeka hadi 35 kufikia jana.

Hiyo ni Kwa mujibu wa taarifa walizopokea awali, baada ya tetemeko la ardhi kutokea mjini Majene.

Tetemeko hilo la ardhi limesababisha watu 637 kujeruhiwa na zaidi ya wengine 15,000 kuhamishwa makazi yao.

Timu ya utafutaji na uokoaji bado inaendeleza juhudi zake katika mkoa huo.

**RFI/TRT**

MAKALA

# Ni watu au maisha ndiyo yamebadilika?



Na Magabilo Masambu

**Leo hata kwenye familia zetu, mwenye fedha ndiye mwenye thamani hata akiwa mdogo kuliko wote, ndiye mwenye kauli, wengine ni wasikilizaji. Mapenzi yetu pia kwa wazazi na watu wetu wa karibu yamebakia kuunganishwa na fedha bila hiyo hakuna mapenzi.**

TAFAKURI ya kina inahitajika ili kutegua kitendawili hiki. Kwamba ni watu au maisha ndiyo yamebadilika? Pengine vijana wa sasa swali hili linaweza kuwa msamiati kwao, kwasababu kama hawakuwahi kuyaishi maisha ya zamani kidogo ni vigumu kutofautisha maisha tunayoishi leo na yale tuliyoishi nyakati zile.

Kwa upande wa pili, watu wenye umri mkubwa sasa na waliopata nafasi pia ya kuishi vijijini na mijini wanaweza kuwa wanaelewa nachozungumza hapa.

Kwa sasa inaonekana kama mioyo ya watu imebadilika sana, ukarimu, utu, ubinadamu, upendo, nakadhalika vinaonekana kama bidhaa adimu siku hizi. Wapo wanaodai kwamba maisha yamebadilika na wapo wanaosema mioyo ya watu imebadilika.

Binafsi sjui ni kipi kimetangulia kubadilika, kati ya watu au maisha. Nachokumbuka sawasawa ni maisha tuliyoishi zamani, japo nilikuwa mdogo, lakini nilikuwa naona jinsi watu walivyokuwa wanachukuliana.

Ushirikiano katika mambo mbalimbali ya kijamii.

Leo mambo hayo yamepungua sana si vijijini wala mijini hali inayo onekana kufanana.

Tofauti ya ushirikiano wa leo na ule wa zamani ni kwamba, ushirikiano wa leo hauwezi kuwepo na kuimarika kama hakuna fedha! Yaani leo ili uwe ndani ya ushirikiano lazima fedha ndiyo kiwe kiunganishi, nje ya hapo hakuna urafiki, udugu, wala umoja.

Leo hata kwenye familia zetu, mwenye fedha ndiye mwenye thamani hata akiwa mdogo kuliko wote, ndiye mwenye kauli, wengine ni wasikilizaji.

Mapenzi yetu pia kwa wazazi na watu wetu wa karibu yamebakia kuunganishwa na fedha bila hiyo hakuna mapenzi. Wanasema hapendwi mtu inapendwa pesa.

Jambo moja tu nimeliona, likanifanya nijaribu kufikiri tulivyokuwa tunaishi zamani.

Siku hizi hata kama mtu ana pikipiki yake binafsi akitokeza barabarani na hafanyi biashara ya bodaboda, lakini ukimsimamisha uombe lifti atakuuliza una shilingi ngapi, kama hauna hautapata lifti!

Vivyo hivyo hata kwenye magari. Leo mtu anakwenda kanisani anawapita waumini wenzake gari likiwa tupu, wanatoka kanisani anarudi bila kumpakiza yeyote kwenye gari na wanatoka kanisani hapo. Kuna wakati tunajitetea kwamba watu siku hizi wamebadilika, unaweza kupakiza jambazi!

Ni kweli, lakini hata majirani zako unaokwenda nao kanisani ni majambazi?

Nakumbuka zamani kwenye familia watu walikuwa wanalelewa na wanapata maisha wakiwa kwenye familia ambazo si zao. Kitu kizuri ni kwamba hata walipofanikiwa hawakusahau kurudisha fadhila kwenye familia hizo kama shukrani za kulelewa, waliishi kama watoto wa familia hizo maisha yao yote.

Lakini leo ni kwa kiasi gani tunapenda kuwa na watu kwenye familia zetu? Wale wanaosaidiwa kwenye hizi familia ni kwa kiasi gani pia wanathamini na kutambua michango hiyo baada ya mafanikio? Je, ni hali ya maisha imekuwa ngumu kutimiza mahitaji ya watu wasio sehemu ya familia? Kuna maswali mengi ambayo sina hakika kama yana majibu ya moja kwa moja.

Ni kweli inawezekana ugumu wa maisha unaweza kuwa umechangia hali hii kujitokeza. Lakini tusikubali kamwe udugu wetu kama Watanzania uendelee kufa taratibu mwisho wake utakuwa mbaya.

Tumeshafikia mahali watu tunaishi nyumba moja, lakini hatufahamiani na wala hatuoni umuhimu wa kufanya hivyo.

Utasikia kila mmoja na mpango wake, mkisalimiana ni kwa bahati mbaya.

Nyumba za mageti. Ni kweli kwamba tunajenga nyumba na kuweka kuta ndefu kwaajili ya usalama wetu, swali, nani anaondoa usalama huo? Jibu ni Watanzania wenzetu. Kwa hiyo kumbe sisi wenyewe tumekuwa hatari kuliko wanyama pori, kiasi cha kuwekeana kuta. Pamoja na usalama huo, lakini lazima tufahamu kwamba tunaendelea kutengeneza kizazi chenye ubinafsi wa hali ya juu na hata usalama wetu unakuwa mdogo kwa sababu ya ubinafsi huohuo.

Nyumba zisizo na kuta ndefu tulipokuwa watoto zilitutwezesha kucheza pamoja na kutufanya tupendane kutokea wadogo na kujenga umoja wetu tukiwa watu wazima. Leo hali ikoje? Mtoto anamjua baba, mama na nduguze tu akiwa kiongozi huyu atawafikiria wengine kweli?

Tujitafakari upya, ni kweli maisha yamekuwa magumu, lakini fedha bado haiwezi kutatua kila kitu. Kwasababu hata wenye fedha nyingi hawajawahi kumaliza changamoto walizonazo, bado wanapambana mpaka kifo kiwakute. Maisha ni hayahaya tutafute polepole huku tukiyafikiria maisha ya wengine pia. Utu na thamani ya binadamu ni kubwa zaidi kuliko fedha.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Dar Jazz ilikuwa Simba, Western Jazz, Yanga



Na Adam Fungamwango

**Nasikia hii ipo hata Afrika Kusini. Pamoja na matatizo yao yote. Lakini mashabiki wa timu pinzani, Orlando Pirates na Kaizer Chiefs nao vile vile wao kama Wazanzibari. Nao pia wakakaa pamoja wakati timu zao zinapambana kwenye 'dabi' yao.**

NILIKUWA naangalia fainali ya Kombe la Mapinduzi mjini Zanzibar. Nilifurahishwa sana na tabia au utamaduni wa watu wa Zanzibar. Maana nasikia hata ustaarabu ulianzia Mashariki na Kati na kuteremka taratibu hadi Visiwani na baadaye ukaingia Bara.

Ni kwamba mashabiki wa Simba na Yanga walikuwa wamechanganyika. Wamekaa sehemu moja. Wanaongea pamoja. Wanafurahi pamoja. Wanakunywa juisi pamoja. Ngoma inapigwa hiyo hiyo ndiyo wanaocheza mashabiki wa Simba na Yanga, wakiwa hapo hapo. Hawagusani, wala kunyoosheana vidole vya macho.

Wameshangilia hadi mechi ilipoisha. Waliotwaa ubingwa wakafurahia kombe lao, na waliofungwa wakarejea majumbani taratibu. Hakukanyagwa hata sisimizi.

Nasikia hii ipo hata Afrika Kusini. Pamoja na matatizo yao yote. Lakini mashabiki wa timu pinzani, Orlando Pirates na Kaizer Chiefs nao vile vile wao kama Wazanzibari. Nao pia wakakaa pamoja wakati timu zao zinapambana kwenye 'dabi' yao. Ni kama mtoko vile wa kifamilia. Wanakaa baba Simba, mama Yanga, watoto nao wamechanganyika, ili mradi tu raha juu ya raha.

Hali hii haipo Bara. Hasa kwa kizazi cha sasa. Wenyewe tayari wamesha-geuza ushabiki wa Simba na Yanga kuwa ni uhasama. Simba na Yanga zikicheza kwenye Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam, shabiki wa timu moja akajichanganya kwenye sehemu nyingine inakuwa ni kama kujitafutia kifo.

Atapigwa, atachaniwa jezi na kupata kila aina ya madhila. Eti mashabiki wa Simba wanakaa kwao na wa Yanga kwao. Hakuna kuchanganyika.

Huko mitaani ngumi zinafumuka. Watu hawataki kutaniwa. Wanataka kutania wao tu.

Hawajui historia ya timu hizi. Moja kati ya sababu ya kuundwa kwa timu hizi, mbali na mambo ya kudai Uhuru, ilikuwa ni kudumisha undugu, upendo na kusaidiana. Pia ilikuwa ni sehemu ya kukutana kwa ajili ya burudani.

Zamani timu moja ikifungwa, basi mashabiki wa timu nyingine watapika hata pilau na kuwaita waliofungwa ili wale. Watanunuliwa na vinywaji, watakuwa wanakula, lakini wanataniwa na kusimangwa. Huo ndiyo utani wa zamani. Siku hizi ni matusi, kejeli na vitisho kwenda mbele. Si kwa aliyeshinda au aliyefungwa. Hakuna aliye mbele wala aliye nyuma. Mwisho wa yote ni ngumi.

Utani wa jadi unaelekea kwisha, unataka kubaki uhasama. Nenda kwenye mitandao ya kijamii. Huyu anatania, lakini wengine wanamtukana. Hawataki kutaniwa. Huu sio ule ushabiki wa zamani wa timu hizo mbili. Zamani ushabiki wa Simba na Yanga haukutofautiana na ule wa makabila mbalimbali ya nchini Tanzania. Hata kwenye msiba wa mashabiki hao, mashabiki wa upande mwingine ndiyo wanaubeba zaidi kuwafariji wenzao.

Nimefurahishwa zaidi na mashabiki wa klabu za Simba na Yanga mkoani Kigoma. Hii si mara ya kwanza wala ya pili kuona. Mashabiki wa Yanga baada ya kushinda Kombe la Mapinduzi, waliwapikia msosi mashabiki wa Simba, wanawanyoa nywele na kuwapaka unga mwili mzima.

Wakawapa chakula wale wakiwa weupe kwa kupakwa unga, huku wakiwa vipara. Hata wa Yanga nao walifanywa hivyo hivyo siku walipofungwa mabao 4-1 kwenye Kombe na Mapinduzi. Huu ni utamaduni mzuri sana na wameurithi kutoka kwa mababu zao.

Kutokana na historia ya nchini hii, wananchi wake wameganyanyika sehemu mbili kuu kwenye masuala ya soka. Ni Simba na Yanga tu. Hata familia zimegawanyika hivyo. Lakini cha ajabu unakuta badala ya kuwa utani unakuwa kama ugomvi, wakati hata nyumbani timu ya upande wa pili wapo.

Utamtukana vipi shabiki wa Simba, wakati mkeo anaipenda timu hiyo hiyo? Unampiga vipi shabiki wa Yanga, wakati nyumbani watoto wako pia ni Yanga?

Zamani hata bendi zilinasibishwa na upenzi wa timu hizo kuu mbili. Dar es Salaam Jazz au Dar Jazz iliyokuwa inatumia mtindo wa 'Majini wa Bahari', 'Dar Sengo' na 'Mundo Kamata' iliyoanzishwa kati ya mwaka 1919 na 1920, ilikuwa ina unasaba na klabu ya Simba, huku Western Jazz wana 'Saboso' iliyoanzishwa mwaka 1944 ikitajwa kuwa na uswahiba na Yanga.

Hata hivyo, haimaanishi kuwa mashabiki wa Simba hawakuwa wanakwenda kusakata rhumba la Saboso, wala wa Yanga kwenda Mundo.

Walikuwa wanachanganyika, wengine huku leo na wengine kesho wanakwenda kule. Hata wanamuziki wa bendi hizo mbili, nao walikuwa timu tofauti, na wala haikulazimisha kuwa mwanamuziki wa Western awe Yanga na wa Dar Jazz awe Simba.

Cha kufurahisha ambacho mashabiki wa kizazi cha sasa inabidi waige ni kuwa, wachezaji wa Simba walikuwa wanakwenda kwenye ukumbi wa klabu ya Yanga kucheza dansi, na wa Yanga pia wanakwenda kwenye klabu Simba kucheza dansi na hakukuwa na uhasama wowote. Sidhani kama leo hii inawezekana. Kuna mahali tunakosea.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risassi zilifanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu. Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini aliyemteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji? Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina jambo langu-5

**Na Adam Fungamwangwo (0716 350534)**

Akili ikaenda mbali zaidi na kudhani kuwa huenda mkewe anamfahamu mtekaji. Kama si hivyo mkewe kuna kitu amefanya ambacho hakifahamu ndicho kimesababisha mtoto atekwe.

"Mimi haiingii akilini. Isijekuwa ni bwana 'ako, alikuwa anakudai mtoto, akaamua kufanya hivyo?" Hatimaye Ben akatapika nyongo.

"Unanitukana ee baba Diana. Yaani umefika sehemu ya kuniona mimi ni mwanamke na kujitembeza huko, halafu nimepata mimba nimekuletea wewe na sasa wananidai mtoto kweli?" Neema alianza kulia.

Neema alilia na mengi. Kwanza hajui hatma ya mtoto wake. Kwa siku ya pili sasa, amelala wapi. Anaishi vipi? Anakula wapi. Yuko hai au? Hii ilikuwa inamfikirisha na kumkosesha raha na kulia mara kwa mara, licha ya kwamba tayari wameshapiga ripoti kwenye kituo cha polisi Keko.

Sasa imekuja hii ya mumewe kutoamini kama ni utekaji wa kawaida au una makandokando ya mapenzi nyuma yake.

Neema anaamini kuwa hakuna kitu kama hicho, kwani hakuwahi kuwa na mpenzi yoyote jijini Dar es Salaam tangu akaingia akitokea Mbeya.

Na hata huko Mbeya, alikuwa na mpenzi ambaye hakuwa anatembea naye kizembezembe hadi kupata ujauzito.

Alipoingia Dar alikutana na Ben na kuishi kwa mwaka mmoja tu kabla ya kufunga ndoa.

"Usilete mkosi baba Diana. Hapa yenyewe hatujui hatma ya mtoto. Nimeumia sana mimi, nalia usiku kucha, wewe nawe unazidi kuniumiza."

Ben alijua amekosea. Lakini hakuwa na la kusema wala la kufanya. Ujumbe ulikuwa umefika.

Neema alikuwa anahitaji kujua hatma ya mtoto wake Diana. Ben hakutaka kujua hatma tu. Alitaka kwenda mbali zaidi. Hata kama atapatikana akiwa hai, lakini alitaka kwenda zaidi ya hapo. Alitaka kujua kwa nini alitekwa. Kwa nini alitekwa yeye akiwa ndani ya mamilioni ya watoto waliopo Dar es Salaam. Nani aliyemteka? Na ana uhusiano gani na mtoto huyo, pamoja na mama yake?

******************************

Kwa siku tatu sasa, akili ya Jerry




**Neema alibakia anacheka tu. "Ndiyo hivyo tena umeshachelewa. Tungekutana miaka mitatu iliyopita, saa hizi ningekuwa mkeo." Alijibu huku akicheka. Ni kicheko ambacho kilikuwa kichungu kwa Jerry. Hakuwa na matumaini tena ya kumpata Neema.**

ilikuwa inafanya kazi zaidi ya uwezo wake wa kawaida. Kazi kubwa aliyoifanya kugundua mtoto wa Neema, ametekwa na kupelekwa wapi.

Alikuwa na uhakika kuwa ni yeye pekee ndiye aliyejua mtoto huyo amepekwa wapi, ukiondoa mwendesha bodaboda ambaye yeye alichokua anajua ni kulikimbiza gari tu. Hakujua mle ndani mna nani na kwa nini yeye aliamua kulifuatilia.

Baada ya hapo hakuna ninachoendelea. Alijiuliza kama aende kupiga ripoti polisi? Wazo hilo kwa sasa hakuliona kuwa la msingi sana kwa sababu yeye si mhusika.

"Ulijuaje kama na wewe siyo mmoja wao?" Ni swali ambalo alilliogopa kutoka kwa askari polisi.

Alichofanya yeye ni msaada. Kilichomsukuma zaidi ni kwa sababu anamfahamu mama wa mtoto. Neema ni mwanamke ambaye amejaa moyoni mwake. Anampenda mno. Tatizo tu ni mke wa mtu. Aliheshimu ndoa yake. Lakini bao haikuwa kigezo cha yeye kutoonyesha upendo kwa msaada kama huo.

Kuna wanaume wanawapenda wanawake. Baada ya kuwatokea na kuambiwa tayari ni wachumba za watu, au ameolewa, basi wanajitenga nao kabisa. Hata salamu hakuna. Hawataki hata kuwasalimia wakati mwingine. Wanawanunia bila sababu. Hata kama alikuwa anamnunulia soda au chakula, anaacha kabisa.

Siyo kwa sababu anaheshimu ndoa yake. Ni hasira tu na wivu wa kuona hatopata kitu tena.

Kwa Jerry haikuwa hivyo. Aliendelea kuwasiliana na Neema, ingawa si kwa kiwango kile cha mwanzo kabla ya kuambia ukweli.

Bado alitoa msaada wa lifti na vitu vingine kama ikihitajika. Ni kwa sababu tu alimpenda tu mwanamke huyo bila hata yeye mwenyewe kujua ampenda kwa sababu gani.

Pamoja na yote hayo, aliheshimu ndoa yake, hivyo hakumrubuni kumsaliti mumewe.

Ni siku ya Jumapili ambayo hakwenda kazini. Alikuwa asubuhi nyumbani. Bado hakuwa amebahatika kuoa. Alishawahi kumwambia Neema kuwa kama ingekuwa hajaolewa, basi ni yeye ndiyo angemuoa.

Neema alibakia anacheka tu. "Ndiyo hivyo tena umeshachelewa. Tungekutana miaka mitatu iliyopita, saa hizi ningekuwa mkeo." Alijibu huku akicheka.

Ni kicheko ambacho kilikuwa kichungu kwa Jerry. Hakuwa na matumaini tena ya kumpata Neema.

Nia yake ilikuwa kwanza kutaka kuongea na Neema kuhusu jambo hile na si mtu mwingine yoyote.

Atakapoongea naye, ndiyo watajua nini cha kufanya.

Wazo la kumpigia moja kwa moja na kumtaarifu jambo lile nalo hakukubaliana nalo.

Ni kwamba huenda mumewe angekuwepo. Halafu angemwambia, wangeweza kufanikisha hayo yote mtoto akapatikana.

Lakini baadaye, mwanaume ni mwanaume tu, siku isiyo na jina mumewe anaweza akamuuliza, yule alikuwa ni nani? Na kwa nini aliamua kufanya kazi hii yote ya hatari? Nia ilikuwa ni ni kutoa msaada huo wote? Na mlikutana naye wapi? Mnajuana naye vipi?.

Hilo ndilo lilimtisha na kumfanya asite kumpiga simu ya moja kwa moja.

Akakumbuka tukio moja ambalo jamaa alifungwa jela miaka 10, lakini mkewe anapigana kufa na kupona kuhakikisha mumewe anatoka. Akatembea na ofisa mmoja mkubwa wa magereza ambaye alimrubuni na kumwambia akifanya hivyo, mumewe atatoka. Na kweli ikawa hivyo. Mke hakumwambia mumewe. Ikawa siri.

Lakini duniani hakuna siri ya watu wawili, mume akajua. Badala ya kufurahi kuwa mkewe amefanya mbinu yeye ametoka kwenye kifungo ambacho angekaa ndani miaka 10, badala yake akakaa miezi minne tu, akampiga mkewe na kumsemea maneno ya dhihaka.

Ingawa ndoa iliendelea, lakini iliumuumiza sana mume. Hiyo ndiyo tabia ya wanaume. Ndiyo maana alihofia. Alichoona kwanza kinachoweza kumsaidia ni kutuma meseji ya salaam.

Ikajibiwa baada ya dakika tano. Akauliza kama mumewe yupo. Akajibiwa ametoka kidogo. Akampigia. Baada ya salamu, Neema alitiririka jinsi alivyoporwa mtoto na sasa ana wiki zima yupo nyumbani.

Jerry hakumwambia chochote juu ya alichokiona, badala yake akamtaka waonane. "Naomba ukiwa na nafasi kesho au kesho kutwa tukutane, tuongee." "Nini tena Jerry?"

"Hilo suala la mtoto. Siyo mana najua aliyemteka, ila naweza kukusaidia jinsi gani ya kufanya ili tujue mtoto yuko wapi."

"Mmmmh, basi kesho asubuhi."

"Lakini naomba jamaa asijue lolote. Tukutane mimi na wewe tu sawa?"

"Sawa Jerry, kama ni kweli, nitashukuru sana."

**INAENDELEA JUMAPILI**



# YUPI BABA MZAZI WA DIAMOND?

UTATA unazidi kuhusu baba halali wa mwanamuziki wa Bongo Fleva nchini, Diamond Platnumz, baada ya mzee Abdul Juma, kutoa ushahidi kuwa mimba ya msanii huyo ilitungwa kinyume na matarajio ya wazazi wote wawili.

Akizungumza kupitia mahojiano yake na Zawadi Mketema, mzee Abdul amesema anashangaa kusikia mama wa Diamond, akisema mtoto huyo si wake na badala yake kupewa Salum Iddy Nyange, ikiwa hatua zote za kutungwa kwa mimba ya Diamond, anazifahamu na anakumbuka mengi.

"Unajua ninashangaa sana, lakini yeye kama kasema mimi sio baba wa Nasib, nakubaliana naye lakini ajue nafahamu hata utungaji wa mimba wa mtoto yule. Alipopata ujauzito wake wote hatukutarajia lakini nilikubali kulea mimba hadi mtoto kwa miaka yote," amesema mzee Abdul.

Amesema yote yanayoendelea kwa sasa inatokana na jeuri ya fedha, lakini kwa upande wake anamuachia Mungu kwa sababu hakuna anachokipata kutoka kwa Diamond Platnumz.

## Chege utauweza mfupa walioshindwa wenzako?

MKONGWE wa muziki wa Bongo Fleva, Chege, amejaribu kufanya kile ambacho wengi kimewashinda kwa kuwakalisha chini na kuwapatanisha Diamond, Ali Kiba na Harmonize.

Kupitia wimbo wake mpya uitwao 'Burudani', Chege katika mashairi yake amesikika akiimba huku akiwataka wasanii hao kumaliza tofauti zao ili kusogeza muziki wa Bongo Fleva.

"Wakati naandika wimbo wa Burudani najua ni kitu ambacho hakiwezekani lakini mawazo yangu yalisimama na kukumbusha watu kupendana, hakuna kitu kizuri kama ukiwa unaongea bado upo hai, kwa hiyo wimbo wangu wa Burudani ulikuwa na lengo la wasanii wenzangu tunatakiwa tuwe na mipaka ya kibinadamu" amesema Chege.



## Stamina aja na Albam yenye ngoma 8

MSANII wa HipHop, Stamina, amesema hivi karibuni anakuja na Albam yake yenye ngoma kali.

Akizungumza katika kipindi cha Planet Bongo ya East Africa Radio, amesema ngoma yake mpya aliyowashirikisha rapa mkongwe Prof Jay pamoja na One Six itakuwamo katika Albam hiyo.

"Ninatoa Album hivi karibuni na itakuwa na nyimbo 8 japo jumla zitakuwa 10 ukijumlisha pamoja na Outro", amesema.



## HABARI MICHEZO

# Klopp: United sio wanyonge

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema Manchester United sio "wanyonge" kuelekea mchezo unaowakutanisha wababe hao wawili wanaoongoza katika msimamo wa Ligi Kuu England, leo Jumapili.

Wekundu hao wanawakaribisha wapinzani wao wa jadi pale Anfield huku wakitambua ushindi utawapa motisha katika kuelekea kutetea ubingwa wao wa EPL.

United wanaelekea kule Merseyside kama viongozi wa ligi, na watakuwa na tofauti ya alama sita endapo watapata ushindi wao wa kwanza pale Anfield tangu mwaka 2016.

"Sisi ni wapinzani, wao ni mabingwa," amesema Kocha Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea mchezo huo.

Lakini kwa upande wake Klopp ameweka wazi United sio wanyonge na hivyo mchezo huo utakuwa mgumu kweli kweli.

"Nimekuwapo England kwa miaka mitano na Manchester United hawajawahi kuwa wanyonge. Hawawezi kuwa. Ipo hivyo," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Siku zote ni timu bora, wachezaji bora, na wana kocha bora. Siku zote wapo hivyo na sasa wanaongoza ligi.

"Hawawezi kuwa wanyonge, lakini tunacheza nyumbani hatujioni kama wageni au vyovyote eti kwa sababu wapo juu yetu. Tunahitaji kumiliki mchezo," aliongeza Klopp.

"Kikubwa ni kwamba tunatakiwa kuingia mchezoni tukiwa na fikra chanya na kuhakikisha kwamba, tunaweza kupata ushindi kwa namna yoyote."





# MOURINHO ASEMA DELE HANA FURAHA

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho amesema kiungo, Dele Alli, hana furaha katika klabu yake hiyo, wakati tetesi mbalimbali zikimhusisha kuihama timu hiyo katika dirisha hili dogo la usajili.

Alli amepoteza namba katika kikosi cha kwanza tangu Mourinho alipochukua mikoba ya kukinoa kikosi hicho msimu uliopita, huku akimtoa kabisa katika mipango yake ya msimu huu.

Kiungo huyo wa England amecheza mechi nne tu katika ligi msimu huu akiwa amecheza jumla ya dakika 74 katika mechi zote.

"Sio kila timu itakuwa na wachezaji wenye furaha katika chumba cha kubadili nguo, labda kocha huyo awe na bahati na miujiza katika mikono yake," alisema Mourinho akinukuliwa na Sky Sport.

"Unaweza kuwa na wachezaji ambao hawana furaha, lakini wanajua wajibu wao ni kufanya kazi, kazi, kazi, lakini kuna ambao hawana furaha na wanadhani sio kazi yao kupambana na kufanya kazi kila dakika kwa ajili ya timu.

"Swali kuhusu kubadilishana Dele na mchezaji mwingine siwezi kulijibu, siko tayari kulijibu, lakini najua jinsi ya kulijibu."

# *Rooney atundika daluga, awa kocha mkuu*

**LONDON,** England

HATIMAYE safari rasmi ya ukocha kwa aliyewahi kuwa nahodha wa klabu ya Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Wayne Rooney imeanza.

Rooney baada ya kurejea England akitoka Marekani kwenye klabu ya DC United, alitua Derby County wakati ikiwa chini ya Kocha Mkuu, Philip Cocu.

Baada ya mambo kutomwendea vizuri Cocu na hatimaye akaondolewa, Rooney alikabidhiwa jukumu la kuongoza timu hiyo kwa muda akiwa kama kocha mchezaji.

Aliiongoza Derby akiwa kama kocha wa muda kwa kipindi kifupi na sasa ametangazwa rasmi kama kocha mkuu wa klabu hiyo.

Kukabidhiwa jukumu la kuwa kocha mkuu kumeendana na kustaafu kucheza soka.

Rooney anatundika daluga akiwa kama mchezaji mwenye heshima kubwa kwenye Timu ya Taifa ya England na Manchester United, na atakumbukwa kwa umahiri wake wa kuzifumania nyavu ambapo anatambulika kama mfungaji bora wa muda wote kwenye timu hizo.

Rooney atasaidiana na Liam Rosenior, Shay Given na Justin Walker katika benchi la ufundi la Derby County.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA HAJIAMINI ATAMBAKIZA GARCIA

Ni baada ya nyota huyo kuhusishwa na mpango wa kurejea Barca ambapo ni klabu...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amekubali kuwa mlinzi, Eric Garcia ambaye ana umri wa miaka 20, anaweza kuondoka Manchester City mwezi huu.

Mchezaji huyo ambaye yuko katika mwaka wa mwisho wa mkataba wake hapo Etihad, ameonyesha nia ya kutaka kuondoka na alikuwa akihusishwa na kurejea kwenye klabu yake ya utotoni ya Barcelona.

Raia huyo wa Hispania kwa sasa anaruhusiwa kuzungumza na klabu yoyote kuhusu mpango wa uhamisho wa msimu wa majira ya joto, lakini kumekuwa na ripoti zinazoonyesha kwamba Barca inaweza hata kukamilisha makubaliano ya uhamisho mwezi huu.

**Guardiola hajui Garcia atakaa kwa muda gani kwenye dimba la Etihad, na alipoulizwa ikiwa uhamisho huo unaweza kutokea, alisema: "Natumaini siyo, lakini labda watu wa Barcelona wanajua zaidi yangu. Sijui ni nini kitatokea lakini labda kitatokea."**

Garcia amerejea tayari kwa pambano dhidi ya Crystal Palace kwenye Ligi Kuu England Jumapili hii, baada ya kurudi mazoezini akimalizana na kuwa karantini kwa sababu ya corona.

Walinzi wa kati wenzake, Aymeric Laporte na Nathan Ake ni majeruhi na mshambuliaji, Sergio Aguero bado anajitenga baada ya kubainika alikuwa karibu wa mtu ambaye amepatikana na virusi vya corona.

Guardiola katika mkutano na waandishi wa habari amesema anadhani Eric atarejea. Pia Nathan na Ayme bado hawajawa sawa, Sergio pia ni changamoto. Wengine nadhani wako sawa.

## ZISIKUPITE

### RICE AGOMBEWA

MANCHESTER United wapo kwenye mbio moja na Chelsea kuwania kumsajili kiungo wa kati wa West Ham, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, msimu ujao. ***(ESPN)***

### MILAN WAMTAKA FIKAYO

AC Milan wanataka kupewa nafasi ya kumnunua mlinzi wa Chelsea na England, Fikayo Tomori ikiwa watamsajili kwa mkopo mwezi huu. Klabu hiyo ya Italia huenda wakalipa karibu pauni milioni 26 kumpata nyota huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Guardian)***

### DRINKWATER KUONDOKA

KIUNGO wa kati wa Chelsea, Danny Drinkwater (30), anakaribia kutia saini mkataba wa mkopo kujiunga na klabu ya Kasimpasa ya Uturuki, baada ya nyota yake kufifia tangu alipotua Stamford Bridge kwa uhamisho wa pauni milioni 35 kutoka Leicester mwaka 2017. ***(Mail)***

### UCHAGUZI WA BARCA

WAGOMBEA watatu wa urais wa Barcelona wamekubaliana kuahirishwa kwa uchaguzi kutoka Januari 24 hadi Machi 7, baada ya masharti mapya ya kukabiliana na virusi vya corona. ***(AS)***

### LACAZETTE KUTIMKA

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, anatafakari uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na Ufaransa, Alexandre Lacazette, baada ya uhusiano wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 29 na kocha wake, Mikel Arteta kuyumba. ***(AS)***

### JOSHUA ANUKIA EVERTON

EVERTON wanataka kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Bayern Munich, Joshua Zirkzee mwenye umri wa miaka 19, na huenda baadaye wakamnunua jumla. ***(Mail)***

### MILITAO KUTUA BAYERN

BAYERN Munich imewasiliana na Real Madrid kuhusu kumsajili mlinzi wa Brazil, Eder Militao ambaye ana umri wa miaka 22, kama mbadala wa David Alaba (30), anayeelekea kujiunga na miamba hao wa Hispania. ***(Goal)***

### BALOGUN AINGIA SOKONI

KUNA timu tatu zinawania kumsajili straika wa Arsenal, Folarin Balogun mwenye umri wa miaka 19, ingawa washikabunduki hao wana matumaini nyota huyo wa England atabadili uamuzi na kusaini mkataba mpya. ***(Guardian)***

### JUVE, ATLETICO VITANI

KLABU ya Marseille ipo kwenye mazunguzo na Napoli juu ya dili la kumsajili straika wa Poland mwenye umri wa miaka 26, Arkadiusz Milik, ambaye pia anawaniwa na Juventus na Atletico Madrid. ***(Goal)***

### BROM YAMWANIA DIAGNE

WEST Brom inawania kumsajili straika wa Galatasaray na Timu ya Taifa ya Senegal, Mbaye Diagne mwenye umri wa miaka 29. ***(Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

## Yanga Princess yaota ubingwa

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuifungwa JKT Queens mabao 2-0, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema kikosi chake sasa kina asilimia kubwa ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara msimu huu.

Lema alisema mechi hiyo iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Mbweni jijini Dar es Salaam ilikuwa ngumu na matokeo mazuri waliyopata katika mchezo huo ni ishara njema ya kufikia malengo yao.

"Ilikuwa mechi ngumu sana, tumefanikiwa kupata ushindi katika mechi hii, basi nina imani ya kuendelea kufanya vizuri zaidi katika mechi zetu zijazo," alisema kiungo huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars).

Naye Kocha wa JKT Queens, Azishi Kondo, alisema wachezaji wake wamefanya makosa na Yanga wametumia nafasi hiyo kuwaadhibu katika mchezo huo.

"Hii ligi ni mbio ndefu na bado mechi zipo nyingi, tumepoteza mchezo wa leo (juzi) dhidi ya Yanga, lakini bado tuko katika mbio za ubingwa, tumeona upungufu wetu na tunakwenda kufanyia kazi," alisema Kondo.

Baada ya mechi hiyo ya juzi, Yanga Princess imeendelea kuongoza katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 25 ikifuatiwa na JKT Queens yenye pointi 21 wakati mabingwa watetezi, Simba Queens wenye pointi 20 wakishika nafasi ya tatu lakini wana mechi moja mkononi.

## Masaka akiwaza kiatu cha dhahabu

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Yanga Princess, Aisha Masaka, amesema anahitaji kuisaidia timu yake kutwaa ubingwa wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania lakini pia yeye kutwaa Tuzo ya Mfungaji Bora.

Masaka ambaye pia ni mshambuliaji nyota wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), juzi alifunga bao moja katika ushindi wa magoli 2-0 walipoifuata JKT Queens na kufikisha idadi ya mabao tisa msimu huu.

Masaka ambaye ametua Yanga Princess msimu huu akitokea Alliance Girls ya jijini Mwanza amesema licha ya ushindani uliopo katika kuwania tuzo hiyo, bado anaamini atatimiza ndoto zake.

"Tunahitaji ushindi katika kila mechi ili kufikia kile kinachotarajiwa wa Wana-Yanga, kwangu nitahakikisha nafunga bao kila mechi ili kufikia malengo niliyojiwekea ya kuwa mfungaji bora," alisema mshambuliaji huyo.

Straika wa JKT Queens, Fatuma Mustapha mwenye magoli 20 ndiye anaongoza kwa kupachika mabao akifuatiwa na Aisha Juma wa Alliance Girls aliyefunga mabao 13 huku Oppa Clement wa Simba Queens yeye amefunga mabao 12.

Washambuliaji wengine waliofunga mabao tisa ni pamoja na Jamila Rajabu wa Baobab Queens ya Dodoma na Hasnath Linus wa Fountain Gate zamani Tanzanite Queens.

# MTIBWA YAWAANGUKIA MAREFA RAUNDI YA PILI

**Na Adam Fungamwangwo**

KLABU ya Mtibwa Sugar imewaomba waamuzi watakaopangwa kuchezesha mechi za raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara kufuata vyema sheria na kanuni ili kupata bingwa wa msimu wa 2020/21 ambaye anastahili.

**Mtibwa Sugar wametoa kauli hiyo huku timu yao ikiwa katika nafasi mbaya kwenye msimamo wa ligi hiyo wakati msimu uliopita iliponea chupuchupu kushuka daraja.**

Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema anawaomba waamuzi wachezeshe kwa haki ili kupata wawakilishi imara watakaokwenda katika mashindano ya kimataifa na pia timu zitakazoshuka daraja basi zishuke kwa kutokana na kufanya vibaya na si vinginevyo.

"Kwanza nawapongeza waamuzi waliochezesha mzunguko wa kwanza. Hakukuwa na malalamiko makubwa sana kama kipindi cha nyuma. Yapo tu yale ya kawaida na ya makosa ya kibinadamu. Ila sasa kwenye mzunguko wa pili, timu zitakuwa zinapigana vikumbo ili zibaki Ligi Kuu, hapo ndipo wanatakiwa wawe makini sana, ili zisije timu ambazo zitataka kufanya ujanja ili kuzishusha zingine kwa hila," alisema Kifaru.

Kuhusu usajili, Kifaru alisema hawakusaka wachezaji wapya wengi katika kipindi hiki cha dirisha dogo, badala yake wameangalia nyota kutoka kwenye vikosi vya timu zao za vijana za umri chini ya miaka 17 na 20 na kuwapandisha.

"Sisi tuna hazina ya vijana, kwa hiyo kwenye kipindi hiki tumepandisha baadhi ya vijana kwa ajili ya kuchezea kwenye klabu yetu kubwa. Timu yetu ndiyo imetoa vijana wengi kwenda kuchezea klabu kubwa kama Shiza Kichuya, Kibwana Shomari, Mzamiru Yassin, Mohamed Ibrahim na wengine wengi," alisema Kifaru.

Aliongeza wanaamini kikosi chao kitaendelea na ligi kikiwa tofauti na kilivyoanza msimu baada ya kuyafanyia kazi upungufu waliyoyabaini.

"Tutarudi kivingine, sisi ndio Mtibwa Sugar, tulianza kwa kusuasua, lakini tutarejea na nguvu mpya, tunajua timu zote zimejiimarisha," Kifaru aliongeza.

Mtibwa Sugar yenye pointi 22 baada ya kucheza mechi 18, iko kwenye nafasi ya 11 wakati Yanga yenye pointi 44 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba wenye pointi 35, lakini wana mechi tatu mkononi.




Baadhi ya mashabiki wa Yanga wakiwapiga picha za video wachezaji wao kwa kutumia simu za mikononi baada ya kuwasili jijini Dar es Salaam hapo juzi wakitokea Zanzibar katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi. Yanga ilitwaa ubingwa wa michuano hiyo kwa kuifunga Simba penalti 4-3. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Luizio, Pastor watua Mbeya City*

**Na Adam Fungamwangwo**

KATIKA kuonyesha Mbeya City haitaki mzaha kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imeongeza wachezaji wapya nane ambao ni wazoefu ili kuhakikisha timu hiyo haishuki daraja msimu huu.

Kipa wa zamani wa Simba na Yanga, Ally Mustapha 'Barthez' na mshambuliaji, Juma Luizio ni baadhi ya wachezaji waliongezwa katika kipindi cha dirisha dogo ambacho kilimalizika juzi usiku.

Katibu Mkuu wa Mbeya City, Emmanuel Kimbe, aliwataja wachezaji wengine ambao wameongezwa kwenye kikosi hicho ni Jamal Mwambeleko, David Mwasa, Yayo Kato, Touya, Jean Didier, Pastor Athanas na Hamisi Thabit.

"Tumeongeza baadhi ya wachezaji kwa matakwa ya kocha wetu ambaye alikuwa anataka wachezaji wenye uzoefu na ligi hii ili kupambana na aina za mechi ambazo zinahitaji wachezaji wa aina hiyo," alisema Kimbe.

Katibu huyo alisema Kibu Denis ambaye ilidaiwa anatakiwa na klabu za Azam FC na KMC bado ni mchezaji wao na uongozi haujafanya uamuzi wa kumuuza kwa sasa mpaka pale watakapopokea ofa nono.

"Huyu (Kibu), yuko kwenye malengo yetu, hatumuuzi na haendi popote. Ila kama tutaona ofa yenyewe ni nono zaidi kiasi kwamba inaweza kutufanya tufikirie vinginevyo sawa, lakini kwa hivi hivi tu, hapana," alisema katibu huyo.

Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama ili kupisha majukumu ya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ambayo kwa sasa iko Cameroon katika mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

# Michezo

Jumapili Januari 17, 2021

Nipashe




Guardiola hajiamini atambakiza Garcia UKURASA 22



Beki tegemeo wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Bakari Mwamnyeto (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji mwenzake wa timu hiyo katika mazoezi yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Centenary, Limbe nchini Cameroon. **PICHA: TFF**

## Kaseja hesabu kwa Zambia

**Na Mwandishi Wetu,** LIMBE

WAKATI nahodha msaidizi wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Juma Kaseja akiamini wako imara kuhakikisha wanaanza vyema fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), dhidi ya Zambia, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Etienne Ndayiragije amesema 'mambo' yatakwenda vizuri.

Zambia maarufu Chipolopolo itaikaribisha Taifa Stars katika mchezo wa kwanza wa Kundi D utakaochezwa kuanzia saa 1:00 usiku keshokutwa kwenye Mji wa Limbe, nchini Cameroon. Kaseja alisema kuwa baada ya kutua Cameroon tayari wachezaji wa Stars wamepata 'joto' la mashindano na wako tayari kupambana kwa ajili ya nchi yao.

Kipa huyo wa zamani wa Simba na Yanga alisema wamewataka wachezaji vijana walioko katika kikosi hicho kutumia vizuri nafasi waliyoipata kwa kufanya vyema na hatimaye kuijengea heshima nchi.

"Tunamshukuru Mungu, kwa sababu kila taifa linahitaji nafasi hii, linatamani kuwa hapa, tulipambana katika mechi ya kwanza dhidi ya Kenya, baadaye Burundi na leo hii tuko hapa, mazoezi yanaenda vizuri, naona jinsi wanavyojitoa, ninaimani Mungu akituamsha salama mechi ya kwanza tunaweza tukapata matokeo," alisema Kaseja.

Aliongeza nyota wakongwe walioko katika timu hiyo wako kwa ajili ya kuwaongoza wenzao ndani na nje ya uwanja ili wafanye vizuri na vile vile watumie nafasi hiyo 'kupigania maisha yao'.

"Tuliokuja huku ni Watanzania, hatujaja kushindana na kina Aishi (Manula), Magore, sisi tumekuja kuwatia moyo, waendelee kufanya vizuri huu ni muda wao, tusapoti timu, tuitangulize Tanzania mbele," Kaseja aliongeza.

Naye Yusuph Mhilu alisema nafasi wanafanya mazoezi ya nguvu kwa ajili ya kujiandaa kupata matokeo mazuri kwenye mechi zilizoko mbele yao na wanawaahidi Watanzania watarajie makubwa.

"Nimejipanga vizuri, tumekuja kutafuta ushindi na kutafuta ubingwa, sisi vijana tumekuja sokoni," alisema Mhilu.

# Simba, Yanga zasubiri muda

**Na Saada Akida**

### ●●● Kila upande wakamilisha hesabu za usajili kwa kunasa majembe yenye viwango na...

VIGOGO wa soka nchini, Simba na Yanga, wametumia vyema dirisha dogo la usajili ambalo lilifungwa rasmi juzi usiku kwa ajili ya kila upande kutimiza malengo ya kufanya vizuri katika msimu wa 2020/21 ambao unaendelea.

**Simba ambayo imetinga hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika imedhamiria kufanya vizuri zaidi katika michuano hiyo lakini pia ikijipanga kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA, mataji ambayo wanayashikilia.**

Wekundu wa Msimbazi ilikamilisha usajili wake kwa kumnasa mshambuliaji wa FC Platinum ya Zimbabwe, Perfect Chikwende, lakini ikitajwa kuwa kwenye hatua za mwisho za kumsajili mshambuliaji Mnigeria kwa ajili ya michuano ya kimataifa.

"Mimi sasa ni mwekundu, mimi ni Simba, nina furaha ya kujiunga na klabu kubwa Afrika," alisema Chikwende baada ya kutambulishwa rasmi na wenyeji hao wa Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wa watani zao, Yanga wenyewe wamekamilisha hesabu zao kwa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Burundi, Fiston Abdulrazack na Dickson Job kutoka Mtibwa Sugar.

Yanga ambayo imetoka kutwaa ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi, imeendelea kujiimarisha ili kuhakikisha inarejesha heshima yake kwa kuwavua Simba taji la Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.

Kikosi hicho kinachoongozwa na Mrundi Cedric Kaze kimeahidi kumaliza ubabe wa Simba na kurejesha mataji Jangwani kwa kufanya vyema na hatimaye kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa hapo mwakani.

"Tunataka kumaliza unyonge, sisi ni Yanga, kama wewe ni shabiki wa Yanga, chukua mkono wako wa kulia na weka kifuani upande wa kushoto na sema mimi ni Yanga, daima mbele, nyuma mwiko," Antonio Nugaz, Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, alisema.

**NKAMIA VS MANGUNGU**

Kamati ya Uchaguzi ya Simba imetangaza majina ya wagombea wawili waliosalia katika kinyang'anyiro cha kuwania nafasi ya uenyekiti wa klabu hiyo katika uchaguzi mdogo unaotarajiwa kufanyika Februari 7, mwaka huu jijini.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Boniface Lihamike aliwataja wagombea hao ni pamoja na Juma Nkamia na Murtaza Mangungu.

Lihamike alisema wagombea hao wamebakia wawili baada ya Rashid Shangazi, Hamisi Tika na Bito Mwakisu kuandika barua za kujitoa kwenye mchakato huo.

"Wajumbe wawili hawakukidhi vigezo ambao ni Hassan Dalali na Mohammed Msoloka, wagombea watano wamepita, kati ya hao Bito aliandika barua ya kujitoa katika kinyanganyiro cha ugombea huo, lakini pia Shangazi na Tika wakajiondoa na kamati imeridhia na kubaki na wagombea wawili," alisema Lihamike.

Alisema wagombea hao wanaruhusiwa kuanzia kampeni leo huku akiwakumbusha atakayekwenda kinyume na katiba ya klabu hiyo atachukuliwa hatua na kamati yake.

Wekundu wa Msimbazi wanafanya uchaguzi mdogo ili kuziba nafasi ya iliyoachwa na aliyekuwa mwenyekiti, Swedi Nkwabi ambaye alijiuzulu nafasi hiyo miaka miwili iliyopita.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 3 4